**NEYMAR** atetewa Brazil
UKURASA 21



**SERIKALI** yailipa fidia bilioni. 76/- kampuni ya madini
UKURASA 2



**KITUO** cha afya chabomoka kabla hakijaanza kazi
UKURASA 8


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumatano Oktoba 18, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581467

www.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper


# LATRA yaonya wamiliki mabasi kupandisha nauli

UKURASA 2

## Manispaa Temeke kumchukulia hatua Katibu Mkuu CWT

UKURASA 7



UKURASA WA 19

## ISRAEL YAKUBALI KUWASILISHWA MSAADA GAZA

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, amesema Israel imekubali kufanya kazi na Marekani...

# SAMIA AKERWA UCHELEWESHAJI MIZIGO BANDARINI



Aziagiza mamlaka husika kujipanga kuepusha kazi kudorora...

Endelea Uk. 3

MICHEZO YANGA KUITUMIA MECHI SIMBA KUIMALIZA AL AHLY UK. 24

KATUNI UK. 6



Rais Samia Suluhu Hassan akifungulia maji baada ya kuuzindua mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria kwa ajili ya Mji wa Shelui katika hafla iliyofanyika Kijiji cha Kizonzo, Wilaya ya Iramba, mkoani Singida jana. **PICHA: IKULU**

# LATRA yaonya wamiliki mabasi kupandisha nauli

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imewaonya watoa huduma ya usafirishaji wa abiria mijini (daladala) kupandisha nauli kinyemela na kuwataka kufuata utaratibu uliowekwa.

Wakati LATRA ikitoa onyo hilo, Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA), kimesema leo kitawasilisha ombi kwenye kikao na mamlaka hiyo la kutaka kupandishwa kwa nauli.

LATRA imeitisha mkutano wa wadau kwa ajili ya kupokea maoni kuhusu marejeo ya nauli za mabasi ya masafa marefu na daladala mkoani Dar es Salaam.

Kwa mujibu wa TABOA, hoja kubwa watakayowasilisha kwenye kikao hicho ni kuomba nauli zipandishwe ili kuwasaidia kumudu gharama ambazo zimepanda ili kuendelea kutoa huduma bila matatizo.

Katibu Mkuu wa TABOA, Priscus Joseph, alisema sababu kubwa ya kuomba kupandishwa kwa nauli ni kupanda kwa mafuta, kuadimika na kupanda kwa dola na kupanda kwa gharama za vipuri vya magari ambavyo asilimia kubwa huagizwa nje ya nchi.

Akizungumza na mwandishi wa habari hii jana, Joseph alisema ni vyema ikiwezekana serikali ibebe jukumu la kupunguza makali ya gharama za mafuta ili kuwapunguzia ukali wa maisha wananchi kwa sababu tayari biashara imekuwa ngumu kwao.

"Hoja yetu kubwa katika mkutano wa kesho (leo) ni kuhusu kuomba mabadiliko ya nauli. Hakuna asiyejua kwa sasa kwamba hali ni mbaya. Mafuta yamepanda, dola imeadimika na imepanda ambayo nayo ni muhimu kwenye sekta hii lakini hata vipuri vya magari navyo vimepanda," alisema Joseph.

"Hali ni mbaya kwa sisi tunaofanya biashara hii ya usafirishaji kwa sasa. Tunaendesha biashara kwa hasara, hivyo ombi letu kubwa katika mkutano wa kesho (leo) ni kuomba nauli ipande. Hali ni mbaya na ni vigumu kuendesha biashara kwa nauli hizi sasa," aliongeza.

Kabla ya TABOA kuweka wazi hoja hiyo jana mchana, tayari LATRA asubuhi yake ilikuwa imetoa onyo kwa baadhi ya watoa huduma hiyo ya usafirishaji wa daladala ambao wanakusudia kupandisha nauli kiholela.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mkuu wa LATRA, Habibu Suluo, wamebaini uwapo wa baadhi ya watoa huduma hiyo ya usafirishaji wa abiria hususani daladala wanaokusudia kupandisha nauli hiyo kiholela.

"LATRA tumebaini uwapo wa baadhi ya watoa huduma ya usafirishaji abiria mijini (daladala), waliokusudia kupandisha nauli za usafiri huo kiholela kwa madai ya kupanda kwa bei ya mafuta ya dizeli na petroli.

"Pamoja na LATRA kukutana na watoa huduma hao kwa kuwaelimisha juu ya utaratibu unaopaswa kufuatwa kisheria, baadhi yao wameonyesha nia ya wazi ya kupinga na wanakusudia kukiuka masharti ya leseni zao kwa kupandisha nauli kiholea. Azma hiyo ni ovu na haikubaliki katika nchi yetu sikivu," alisema.

**LATRA imeitisha mkutano wa wadau kwa ajili ya kupokea maoni kuhusu marejeo ya nauli za mabasi ya masafa marefu na daladala mkoani Dar es Salaam.**

Alisema tayari mamlaka hiyo imeanza kushughulikia maombi ya watoa huduma hiyo ya usafirishaji kwa kufanya mrejesho wa nauli za sasa.

"Kwa mujibu wa Kanuni za Leseni za Usafirishaji Mabasi ya Abiria za mwaka 2020, Tangazo la Serikali namba 76 la Julai 2, 2020, ni kosa kutoza nauli zaidi ya kiwango kilichoinidhinishwa na mamlaka.

"Amri ya LATRA iliyotangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 8 la Mei 6, 2022, iliweka viwango vya nauli kwa mabasi ya mijini (daladala) ambavyo havijabadilika," alisema Suluo.

Mkurugenzi huyo alitaja viwango hivyo vya nauli ambavyo ndivyo bado vinatumika kuwa ni Sh. 500 kwa umbali usiozidi kilomita 10, Sh. 550 kwa kilomita kati ya 11 na 15, Sh.600 kwa kilomita 16 hadi 20, Sh. 700 kwa kilomita 21 hadi 25, Sh. 850 (kilomita 26 hadi 30), Sh.1,000 (kilomita 31 hadi 35) na Sh.1,1000 kwa kilomita 36 hadi 40 huku nauli kwa mwanafunzi ikiwa Sh. 200.

"Mamlaka inawatahadharisha watoa huduma waliokusudia kujipangia na kujitangazia nauli holela, kinyume cha sheria na kanuni za usafirishaji, wasitishe kusudio lao na wasubiri matokeo ya mchakato unaoendelea wa kufanya marejeo ya nauli hizi alisema.

Saluo aliongeza kuwa: "Mamlaka itaendelea kutoa elimu kwa umma na haitasita kuchukua hatua stahiki kwa mtoa huduma yeyote au kundi la watoa huduma watakaobainika kukiuka masharti ya leseni zao."

## Serikali yailipa fidia bil. 76/- kampuni madini

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imethibitisha kuilipa kampuni ya uchimbaji wa madini ya Winshear Gold Corp Dola za Marekani milioni 30 (Sh. bilioni 76.5), kama fidia baada ya kuifutia leseni ya mradi wa madini ya dhahabu ulioko Chunya mkoani Mbeya.

Awali, serikali ilidai kuchukua uamuzi wa kufuta leseni hiyo baada ya kurekebisha Sheria ya Madini ya mwaka 2010.

Marekebisho hayo, pamoja na mambo mengine, yalifuta msingi wa kisheria wa leseni hodhi kwa kuvifuta vifungu vya 37 na 38 vya sheria hiyo.

Kutokoana na uamuzi huo wa serikali, kampuni hiyo ilifungua kesi katika Kituo cha Kimataifa cha Usuluhishi wa Migogoro (ICSID) ikitaka ilipwe Dola za Marekani milioni 92 (Sh. bilioni 260) kama fidia.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Jaji Dk. Eliezer Feleshi, alisema serikali imeilipa kampuni hiyo kiasi hicho cha fedha kutoka dola milioni 92 ilizokuwa inadai awali baada ya kukaa na kukubaliana nje ya mahakama.

Jaji Feleshi alisema sheria za ICSID zinaruhusu mshtaki na mshtakiwa kukaa na kufanya mazungumzo nje ya mahakama na kama wataelewana wanaweza kumaliza mgogoro bila kusubiri uamuzi wa mahakama hiyo.

Alisema mpaka wanawalipa fedha hizo na kumaliza mgogoro huo, walikuwa katika kipindi cha kusubiri uamuzi wa mahakama ambacho huchukua miezi sita.

Jana, kupitia tovuti yake, kampuni hiyo ilisema serikali ilitoa Dola milioni 30 kama stahiki, hivyo kumaliza mgogoro uliokuwa ukiendelea kati ya pande hizo mbili.

Taarifa hiyo ilisema baada ya kukatwa gharama zake za kisheria kutoka kwenye malipo hayo, kampuni hiyo imebakiwa na Dola milioni 18 sawa na takribani Sh. bilioni 46.

Taarifa hiyo ilimnukuu Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo, Richard Williams. Akisema: "Suluhu hii ni nzuri kwa Tanzania na Winshear na tunafurahi kufikia hitimisho linalokubalika. Ni wakati wa pande zote mbili kusonga mbele. Tunaitakia Tanzania mafanikio katika kuvutia uwekezaji mpya."

Hii si mara ya kwanza kwa serikali kulipa fidia kutokana na mabadiliko ya sheria hiyo. Julai 14, 2023 ICSID ilitoa uamuzi wa kuitaka serikali kuilipa kampuni ya Indiana Resources Ltd ya Australia takribani Sh. bilioni 250 baada ya kujiridhisha uwapo wa ukiukwaji wa mkataba wa uwekezaji katika Mradi wa Nikeli wa Ntaka Hill mwaka 2018.

**KAULI YA TLS**

Akizungumzia suala hilo, Rais wa Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS), Wakili Harold Sungusia, aliipongeza serikali kwa uamuzi wa kumalizana na mwekezaji huyo nje ya mahakama na kwamba hali hiyo imesaidia kupunguza gharama ilizotakiwa kulipa.

Sungusia aliwashauri viongozi wa serikali kufuata na kusimamia misingi ya utawala bora na sheria wanapokuwa wanatoa uamuzi wa kusitisha mikataba na wawekezaji kwa kuwa wakifanya hivyo kwa kutaka sifa kutoka kwa wananchi, wanaiumiza serikali.

Alisema serikali inaingia kwenye migogoro na wawekezaji kwa sababu baadhi ya viongozi wa kisiasa hushindwa kusimamia misingi ya utawala bora badala yake hulenga kutafuta sifa na kujulikana majukwaani bila kufikiria madhara ya vitendo hivyo.

"Kwa mfano unaweza kukuta kiongozi anasimama jukwaani anasema mwekezaji huyu amechukua ardhi ya wananchi. Anauliza arudishe au asirudishe? Wananchi wanasema arudishee. Hapo anasema kuanzia sasa hivi nabatilisha hati yake," anasema.

Mwanasheria huyo mbobevu alisema sababu nyingine inayoiingiza serikali kwenye matatizo hayo ni sheria dhaifu zilizojikita kuilinda serikali pekee badala ya pande zote mbili, hivyo kesi zinapofika katika mahakama za kimataifa, nchi inashindwa kesi na kutakiwa kulipa fedha nyingi kama fidia.

# Ajali yaua watano, watatu wadhaniwa ni familia moja

**Na Moses Ng'wat,** TUNDUMA

WATU watano, wakiwamo watatu wanaodhaniwa kuwa ni wa familia moja wamefariki dunia kwenye ajali iliyosababishwa na lori lililobeba abiria kufeli breki na kugonga gari dogo na bajaji katika barabara kuu ya Tanzania na Zambia eneo la mteremko wa mlima Chengula mjini Tunduma.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Theopista Mallya, jana alithibitisha tukio hilo kutokea jana majira ya saa 9:30 alasiri.

Akielezea tukio hilo, alisema lori lilikuwa likitokea mjini Tunduma kuelekea Mbeya na lilikuwa likiendeshwa na dereva ambaye jina lake halijafahamika na alikimbia baada ya kugonga gari dogo na bajaji.

Kamanda Mallya alisema kuwa, lori hilo lenye namba za usajili T.468 BUM na trela lenye namba za usajili T. 262 CBR aina ya Scania, baada ya kufeli breki liligonga gari dogo lenye namba T.500 DWN aina ya Toyota Vanguard, lililokuwa likiendeshwa na Elikana Kayungilo (38), mkazi wa Vwawa na kwenda kugonga bajaji namba MC 574 DLW aina ya TVS iliyokuwa ikiendeshwa na dereva ambaye hajafamika na kufariki papo hapo.

Alisema abiria wote watatu ambao wanadhaniwa kuwa ni wa familia moja waliokuwa kwenye bajaji hiyo walipoteza maisha.

Aliwataja marehemu hao kuwa ni Faustina Hala (50), Vicent Mapunda (25) na Venance Faustini (25), ambao anadaiwa kuwa ni mapacha waliokuwa wakijishughulisha na kazi za ufundi seremala, wote wakiwa ni wakazi wa Mpemba, mjini Tunduma.

Aidha, Kamanda Mallya alisema marehemu wengine wawili ambao ni dereva wa bajaji na utingo wa lori hawajatambuliwa na miili yao imehifadhiwa katika kituo cha afya Tunduma.




Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya CRDB, Dk. Ally Laay (kushoto) akimshuhudia Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela akisaini mkataba wa mkopo wa Dola za Marekani milioni 150 uliowezeshwa na Benki ya Intesa Saopaulo na Benki ya Investec. Wa kwanza kulia ni Mkuu wa Masuluhisho ya Mikopo kwa Afrika kutoka Investec Bank, Rowan King pamoja na Mkurugenzi wa Mikopo ya Pamoja Intesa Sanpaolo, Gustaaf Eerenstein. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Samia akerwa ucheleweshaji mizigo bandarini

**Na Waandishi Wetu**

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan ameziagiza mamlaka zote zinazohusika na miradi inayohusisha uagizaji wa vifaa kutoka nje ya nchi zijipange ili vifaa vinapofika visiwe vinacheleweshwa kutolewa bandarini na kusababisha miradi kuchelewa kutekelezwa.

Alitoa agizo hilo jana katika siku ya mwisho ya kuhitimisha ziara yake ya siku tatu mkoani Singida, wakati akizungumza na wananchi wa tarafa ya Shelui, wilayani Iramba, mkoani Singida kwenye mkutano wa hadhara baada ya kuzindua mradi wa maji wa Tinde-Shelui ambao unachukua maji kutoka Ziwa Victoria, utakaonufaisha wananchi zaidi ya 40,000.

Rais Samia alisema kumekuwa na ugonjwa wa kukosekana kwa uratibu ndani ya taasisi za serikali hali inayosababisha kuchelewa kuanza miradi hususani ile inayohitaji vifaa kutoka nje kwa sababu vifaa hivyo vinapoingia nchini vinacheleweshwa bandarini.

"Nilipokuwa India kwa ziara maalum nilipata nafasi ya kuongea na mkandarasi na wataalam wa mradi huu wa maji, walinieleza changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa mradi huu wa maji kuwa ni ucheleweshaji misamaha ya kodi, ucheleweshaji wa vibali vya kazi vya wataalam na washauri pamoja na ucheleweshaji wa kutoa vifaa bandarini," alisema.

Rais Samia alisema kimsingi changamoto zote hizo zinasababishwa na serikali yenyewe na kuagiza sasa ifike mwisho taasisi ziweke utaratibu mzuri ambao utarahisisha vifaa vya mradi vinapoletwa kutoka nje vitolewe haraka bandarini ili kuharakisha utekelezaji wa miradi.

Alisema baada ya maji kutoka Ziwa Victoria kufika Mkoa wa Singida ni jukumu la Wizara ya Maji, watalaam na wahandisi kuongeza kasi ya usambazaji maji kwa wananchi pamoja na kufunga mita ili kuondoa malalamiko yanayotolewa na wananchi kuwa wanabambikiwa bili za maji.

Awali Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, alisema mradi huo unatekelezwa kutokana na Sh. bilioni 40 zilizokuwa zimebaki katika mradi mkubwa wa kuchukua maji kutoka Ziwa Victoria na Sh. bilioni zimetumika kufikisha maji katika Jimbo la Iramba.

"Ndoto yetu kubwa ilikuwa ni kuyatoa maji Ziwa Victoria kuyapeleka Dodoma, lakini tukaona kabla hayajafika Dodoma yafike Singida," alisema.

Meneja wa Wakala wa Usambazaji wa Majisafi na Usafi wa Mazingira (RUWASA) Mkoa wa Singida, Lucas Said, alisema mradi huo utawanufaisha wananchi wa vijiji 12 na zaidi ya watu 500,000 mkoani humo watanufaika na mradi huo.

**VIJANA KUJENGEWA UJUZI**

Akiwa mkoani Tabora, Rais Samia alisema serikali imedhamiria kujenga na kukuza ujuzi kwa vijana kwa kuwekeza zaidi ujenzi wa vyuo vya amali na ujuzi lengo likiwa ni kuwapa fursa kushiriki kikamilifu miradi mbalimbali inayotekelezwa ndani na nje ya nchi inayowahitaji katika ujuzi wa aina mbalimbali.

Alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na wananchi mkoani Tabora baada ya kuweka jiwe la msingi katika Chuo cha Mafunzo ya Amali na Ujuzi (VETA) kilichogharimu zaidi ya Sh. bilioni 2.6.

Alisema serikali inatarajia kujenga vyuo vya Veta katika wilaya zote nchini na chuo kimoja chenye hadhi ya chuo cha mkoa kila Mkoa lengo likiwa kuwawezesha vijana kuwa na ujuzi katika shughuli mbalimbali za kilimo,ufugaji pamoja na ufundi stadi ili waweze kuajiriwa na kujiajiri.

Alisema alisema ili kuondoa tatizo la vijana kuajiriwa katika kazi zenye hadhi za chini, serikali inaendelea na ujenzi wa vyuo 64 kila wilaya.

"Lengo la serikali ni kwenda kufundisha ujuzi zaidi na siyo nadharia kama wanazozipata shuleni kuna miradi mingi inakuja nchini kwetu...," alisema Rais Samia.

Alisema serikali inahitaji kila kijana aende apate mafunzo ya amali na ujuzi katika eneo la nyumbani ili aweze kuzitumia vyema rasilimali zilizopo karibu naye kujiinua kiuchumi ikiwa ni pamoja na kujiajiri na kuajiriwa.

Katika hatua nyingine Rais Samia alisema serikali ina mpango wa kuendelea kutoa fedha za ruzuku kwa wakulima mpaka ifikapo 2025 ili kuwawezesha wakulima kupata pembejeo zenye bei nafuu na bure katika baadhi ya maeneo.

Alisema mpango huo unalenga kuwaongezea uwezo wakulima wapate pembejeo nyingi zaidi ili walime kwa wingi, wapate mazao mengi zaidi na kuuza mazao yao kwa bei nafuu.

"Serikali inaendelea na juhudi mbalimbali na nadhani kwa sasa mmeanza kuona matokeo kwa mfano mbaazi tumetoka kuiuza kwa Sh. 200 kwa kilo, lakini mwaka huu tumeuza kwa Sh. 3,000 kwa kilo katika maeneo tofauti, kazi yetu serikali ni kutafuta masoko ya mazao yatakayolimwa," alisema.

Aidha aliahidi kuwa kama masoko ya mazao husika yatakosekana serikali inajiandaa kununua mazao yote na kuyaweka stoo huku ikiendelea kutafuta wanunuaji.

Awali, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, alimpongeza Rais Samia kwa kuendelea kuidhinisha fedha katika sekta ya elimu ikiwa ni pamoja na mpango wa ujenzi wa vyuo vya Veta kila mkoa na kila wilaya.

Alisema kuwa katika Mkoa wa Tabora, wilaya tano tayari zina vyuo hivyo.

Mkuu wa Mkoa wa Tabora Balozi, Dk. Batilda Burian akieleza fedha zilizotolewa na serikali mkoani humo kwaajili ya miradi ya maendeleo alisema umepokea jumla ya Sh. trilioni 14.7 katika miradi yote ya maendeleo.

Alitaja mkoa huo kuwa wa pekee uliopokea fedha nyingi kutoka serikalini na kueleza kuwa fedha hizo ni kwaajili ya miradi sekta za afya, Sh. bilioni 26, elimu Sh. bilioni 87, nishati Sh. biloni 353, miundombinu Sh. bilioni 319, mifugo Sh. bilioni 1.2 na maji Sh. bilioni 257.

***Imeandikwa na Thobias Mwanakatwe (IRAMBA) na Vitus Audax (TABORA)**

# Wataalam washauri dawa mseto kunywa na maziwa

Na Maulid Mmbaga

WATAALAMU wa afya wameshauri Watanzania kutumia dawa za kutibu ugonjwa wa Malaria aina ya mseto (jina maarufu) na maziwa freshi ama mtindi kwa mwenye uwezo, kwa kuwa yanasaidia mwili kuchukua dawa hizo kwa urahisi zaidi na kuzitumia kutibu ugonjwa huo.

Mfamasia wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Kitengo cha Mloganzila, Marcus Johansen, akizungumza na chombo kimoja cha habari jana jijini Dar es Salaam, alishauri mtu anapopokea dawa hospitalini ni vizuri aulize matumizi sahihi ya dawa husika ili apate ushauri wa kitaalamu utakaomsaidia kupona kwa haraka.

Pia alibainisha kuwa katika matumizi ya dawa za kutibu magonjwa ya maambukizi yakiwamo ya fangasi, kama Afro Conazo na Griseofulvin ili iwe bora zaidi wanashauri mgonjwa asitumie maji kumeza dawa hizo badala yake atumie maziwa kwa kipindi chote cha matumizi.

"Tunashauri hivyo kwa sababu hiyo inasaidia mwili kuzichukua dawa kwa urahisi, au akinywa hizo dawa na maji alafu mapema zaidi akanywa maziwa inasaidia mwili kuzibeba kwa urahisi na kuzipeleka sehemu mbalimbali za mwili zinakotakiwa kwenda kufanya kazi," alisema Johansen.

Aidha, alibainisha kuwa mgonjwa anayetumia dawa zinazotibu magonjwa ya maambukizi kama bakteria au Maambukizi ya Njia ya Mkojo (UTIs) na kutumia Ciprofloxacin, Doxycycline au Tetracyclene, kama ni vidonge vya kumeza, anashauri kwamba hizo ni dawa ambazo mgonjwa hatakiwi kutumia na maziwa kabisa.

Alifafanua kwamba hiyo ni kwa sababu maziwa yana madini kama Calcium na Magnesium, ambayo yakiingia tumboni na kukutana na dawa hizo ambazo nazo zina madini yake zikikutana pamoja zinatengeneza kitu wanachokiita 'Complex compound' kitu kigumu.

"Hiki ni kitu ambacho kinakuwa ni kigumu na mwili hauwezi kukichukua, na kikawa kwenye mfumo wa mmeng'enyo wa chakula na kuingiza katika mfumo wa mzunguko wa damu, kwahiyo maana yake mtu anakuwa yale maziwa aliyokunywa yatapotea lakini hata dawa pia haitafanya kazi yake," alifafanua Johansen.

Hata hivyo, alishauri ili kuepukana na magonjwa ni vizuri watu wakajiepusha na vitu vitamu, akieleza kuwa ni bahati mbaya zaidi kwamba vyakula vitamu ndivyo watu wanavipenda, kuliko ambavyo sio vitamu anavyovitaja ndio bora zaidi kwenye mwili, licha ya wengi kutovipenda.

"Ukimwambia mtu ale magimbi, mihogo au viazi vya kuchemsha, sio rahisi, ukimuambia mtu anywe juisi ambayo haijawekwa sukari kabisa wengi hawawezi lakini ndio chakula bora, kwa sababu sukari hii ya viwandani tunaitumia kwa sababu ya kuongeza utamu tu hakuna kingine cha ziada," alibainisha Johansen.


**BANI INVESTMENT LIMITED**

**DEBT COLLECTORS/ AUCTIONEERS**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **BENKI YA STANBIC** tutauza kwa njia ya mnada wa hadhara mali zilizoorodheshwa hapo chini kama ratiba inavyoonyesha.

| JINA LA MKOPAJI/MMILIKI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA | MUDA |
|---|---|---|---|---|
| KULAR ENTERPRISES | Nyumba iliyopo kwenye PLOT No.27,Block '6' | Mivumoni-Kinondoni Municipality | 4.11.2023 | 4:00 asubuhi nakuendelea |
| LAKE VIEW LIMITED | Nyumba iliyopo kwenye PLOT No.446,Block 'A' | Pasiansi-Mwanza municipality | 11.11.2023 | 3:00 asubuhi nakuendelea |
| LAKE VIEW LIMITED | Nyumba iliyopo kwenye PLOT No.71,Block 'M' | Pasiansi-Mwanza municipality | 11.11.2023 | 5:00 asubuhi nakuendelea |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mali zitauzwa "kama zilivyo " as is where is basis"
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa 25% ya bei iliyofikiwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la 75% katika muda uliopangwa hapo juu hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, kutwaa nyumba/kumtoa mmiliki wa awali (ikiwa bado hajatoka hadi wakati wa mnada) na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wowote isipokuwa usiku.

**Kwa maelezo zaidi wasiliana na Ofisi ya:**

BANI INVESTMENT LTD Nkurmah Street, Lida Building, Ghorofa ya 3, Chumba No. 0313 S.L.P 71340 Dar es Salaam au kwa simu na. 0713 224578,0713 295747(kwa nyumba ya Dar Es Salaam)na 0673 020867,0713 295747(kwa nyumba za Mwanza)



Summons to an Accused Person (S.19)

Criminal Form No. 3 (Approved by the High Court Under Sec. 382 of Criminal Procedure Code

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF SIMIYU

(AT BARIADI)

CRIMINAL CASE NO. ........04........ OF 2023

THE REPUBLIC

VERSUS

PATRICK SAMBALYA MIHAMA ................................ ACCUSED PERSON

To:

Patrick Sambalya Mihama
Plot No. 398, Block A, Sima Area
Bariadi Town Council
Simiyu Region

WHEREAS your attendance is necessary to answer to a charge on ENGAGING UNREGISTERED PERSON OR FIRM TO UNDERTAKE CONSTRUCTION WORKS CONTRARY TO SECTION 22(4) OF THE CONTRACTORS REGISTRATION ACT, CAP. 235 OF THE LAWS

YOU ARE HEREBY COMMANDED IN THE name of the Republic to appear in this Court on the ...27th... day of ...October...... 20.23.... at 08:00 am Or so soon thereafter as the case can be heard.

Here in fail not.

GIVEN under my hand and the Seal of the Court this ....13th....day of ..October...... 2023 ......

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE I/c
................ SIMIYU ................
RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE'S COURT SIMIYU - TANZANIA

This summons has been issued on the Application of the Prosecution

Served Upon Me/us:
Name ..........................................
Signature ..........................................
Qualification/Relationship
Date ..........................................


# Rushwa ya ngono utumishi wa umma yatungiwa mwongozo

Na Beatrice Shayo

SERIKALI imeandaa mwongozo wa ujumuishwaji wa jinsia kwenye utumishi wa umma kwa ajili ya kudhibiti uonevu na ukatili wa kingono katika ofisi za umma.

Hayo yalisemwa jijini Dar es Salaam na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, wakati wa uzinduzi wa mwongozo wa ujumuishaji wa jinsia katika utumishi wa umma na ufunguzi wa mafunzo ya wanawake awamu ya tatu na nne.

Alisema katika maeneo kadhaa ya taasisi za umma, waathirika wakubwa wa vitendo vya unyanyasaji ni wanawake kutokana na jinsia yao.

"Kumekuwa na matukio mbalimbali ya kutowatendea haki ikiwamo kutokupata stahiki zao kwa wakati, kutokupewa nafasi za kujiendeleza, kukosa likizo na nauli ya likizo, madai ya muda mrefu kwa watumishi na unyanyasaji wa kijinsia mahali pa kazi," alisema.

Aidha, katika nyakati tofauti wameshuhudia udhalilishaji na uonevu ambao kwa kiasi kikubwa umewafedhehesha watumishi na kutweza utu wao.

Alisema suala la jinsia linajumuishwa katika maeneo yote na kuakisi hali halisi ya mazingira bora ya utendaji wa kazi kwa watumishi wa umma na waajiri wao nchini, serikali imeona kuunganisha nguvu ya pamoja kudhibiti matendo yasio na haki.

Aidha, matarajio ya serikali ni kuona mwitikio mkubwa kwa waajiri kuzingatia ujumuishwaji wa masuala ya jinsia katika michakato yote ya usimamizi wa rasilimaliwatu tangu mtumishi anapoajiriwa hadi utumishi wake unapokoma.

Alisema lengo ni kuimarisha utendaji kazi kwa kuwezesha na kutoa fursa kwa watumishi wote katika uendelezaji wa rasilimaliwatu,



kuwaandaa na kuwaendeleza watumishi kwa kuzingatia mpango wa urithishanaji madaraka kulingana na mahitaji ya taasisi.

Simbachawene alisema baada ya kuzinduliwa kwa mwongozo huo matarajio yake ni kuona mwitikio mkubwa wa waajiri wote Tanzania Bara kwenye kutekeleza na kupanga bajeti kila mwaka wa fedha ili kumwezesha mratibu wa masuala ya jinsia wa taasisi husika kutekeleza majukumu yake.

Aliwataka waajiri wote katika utumishi wa umma kuelewa vyema na kutekeleza mwongozo wa ujumuishwaji wa jinsia katika utumishi wa umma.

Pia, amezitaka mamlaka zote za ajira Tanzania Bara ziandae mpango kazi wa namna ya kutekeleza afua za usimamizi masuala ya jinsia mahali pa kazi katika utumishi wa umma kama ilivyoainishwa katika mwongozo.

Alisema wanufaika wa programu hiyo watakapomaliza mafunzo yao wakawe mabalozi wazuri kwa kubadilishana maarifa na ujuzi kwa viongozi wengine hasa chipukizi.

Mkuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Dk. Joyce Nyoni, ambaye alimwakilisha Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Doroth Gwajima, alisema kwa miaka ya nyuma uwakilisha wa wanawake katika nafasi za uongozi na ngazi za maamuzi ulikuwa hauridhishi.

Aliipongeza wizara ya utumishi kwa kuandaa muongozo huo akiamini ukitekelezwa utasaidia kuwapo na usawa na kuongeza usimamizi wa rasilimaliwatu katika utendaji wao wa kazi bila kujali jinsia zao.

Alisema wizara yake itaendelea kuhakikisha masuala ya kijinsia yanapewa kipaumbele na kuendelea kutoa elimu pamoja na kutatua changamoto za unyanyasaji wa kijinsia nchini.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi, Kadari Singo, alisema mafunzo hayo yamelenga kuwajengea uwezo katika utendaji wao wa kazi na kufanya maamuzi sahihi.

Alisema kongamano la tatu la wanawake katika uongozi walipokea maombi kwa watu 800 na baadhi yao wanatoka nje ya nchi waliochaguliwa ni 100 wa nchini.

TANGAZO

# tigo pesa — Ni Zaidi ya Pesa

## Ada za wateja. Piga *150*01#

| Kiwango (Tsh) | | Kutuma pesa kwenda Tigo Pesa | Kutuma pesa kwenda Mitandao washirika | Kutoa pesa kwa Wakala/ATM | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzia | Mwisho | Ada ya Tigo Pesa | Ada ya Tigo Pesa | Ada ya Tigo Pesa | Tozo ya Serikali | Jumla ya Makato |
| 100 | 999 | 15 | 15 | - | 10 | 10 |
| 1,000 | 1,999 | 30 | 45 | 300 | 10 | 310 |
| 2,000 | 2,999 | 30 | 45 | 400 | 10 | 410 |
| 3,000 | 3,999 | 50 | 90 | 600 | 14 | 614 |
| 4,000 | 4,999 | 60 | 90 | 650 | 27 | 677 |
| 5,000 | 6,999 | 130 | 180 | 950 | 54 | 1,004 |
| 7,000 | 9,999 | 150 | 180 | 1,000 | 56 | 1,056 |
| 10,000 | 14,999 | 360 | 495 | 1,450 | 102 | 1,552 |
| 15,000 | 19,999 | 360 | 495 | 1,450 | 195 | 1,645 |
| 20,000 | 29,999 | 380 | 540 | 1,850 | 306 | 2,156 |
| 30,000 | 39,999 | 400 | 612 | 1,850 | 351 | 2,201 |
| 40,000 | 49,999 | 410 | 675 | 2,350 | 419 | 2,769 |
| 50,000 | 99,999 | 720 | 1,125 | 2,700 | 573 | 3,273 |
| 100,000 | 199,999 | 1,000 | 1,440 | 3,650 | 707 | 4,357 |
| 200,000 | 299,999 | 1,200 | 1,710 | 5,300 | 821 | 6,121 |
| 300,000 | 399,999 | 1,500 | 2,070 | 6,500 | 838 | 7,338 |
| 400,000 | 499,999 | 1,500 | 2,250 | 7,000 | 982 | 7,982 |
| 500,000 | 599,999 | 2,200 | 2,880 | 7,500 | 1,245 | 8,745 |
| 600,000 | 699,999 | 3,300 | 3,870 | 8,000 | 1,532 | 9,532 |
| 700,000 | 799,999 | 3,300 | 3,870 | 8,000 | 1,700 | 9,700 |
| 800,000 | 899,999 | 3,500 | 3,870 | 8,000 | 1,750 | 9,750 |
| 900,000 | 1,000,000 | 3,500 | 5,400 | 8,000 | 1,776 | 9,776 |
| 1,000,001 | 3,000,000 | 5,000 | 5,400 | 8,000 | 1,875 | 9,875 |
| 3,000,001 | 10,000,000 | 5,000 | 5,400 | 10,000 | 2,000 | 12,000 |

| Tukio | Kuanzia | Mwisho | Ada |
|---|---|---|---|
| Kuweka pesa | 1,000 | 5,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwa mteja ambaye hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | Ada ya kutuma + Ada ya kutoa |
| Kutoa pesa kwa mteja ambaye hana akaunti ya Tigo Pesa au akaunti ya mitandao washirika | 1,000 | 1,000,000 | BURE |
| Kutuma pesa kwenda nchi za nje | 100 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |
| Malipo kwa Tigo Pesa | 500 | 5,000,000 | Kulingana na kiwango |

| Tukio | Ada |
|---|---|
| Kubadilisha namba ya siri | BURE |
| Kuangalia salio/ Taarifa ndogo | 50 |
| Kurudisha muamala uliokosea (Jihudumie) | 50 |
| **Kupata taarifa ya mwezi** | **Ada** |
| Taarifa ya Mwezi jana/Mwezi huu | BURE |
| Taarifa ya Miezi 3 | 1,000 |
| Taarifa ya Mwaka 1 | 2,000 |

Kwa vigezo na masharti ya huduma tembelea tovuti: https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-standard-terms-and-conditions. **Ada zote zimejumuisha kodi zote zinazohusika**
Kwa Ada za huduma nyingine tembelea **tovuti; https://www.tigo.co.tz/tigo-pesa-tariffs**

Furahia Malipo kwa Tigo Pesa:

**KUMBUKA:**

1. Unaweza kuweka au kupokea hadi TSh 10,000,000 kwa siku na unaweza kutoa au kutuma hadi TSh 5,000,000 kwa siku, pia unaweza kuhifadhi hadi TSh 10,000,000 kwa wakati mmoja kwenye akaunti yako ya Tigo Pesa, kama usajili wako umekamilika.
2. Onesha kitambulisho chako kabla ya kuweka au kutoa pesa kwa Wakala.
3. Hakikisha taarifa zako za usajili ni sahihi kwa kupiga *106# kisha 2 au piga huduma kwa wateja kwa maelezo zaidi.
4. Hesabu pesa zako na hakikisha salio lako la Tigo Pesa linaendana na muamala uliofanya kabla ya kuondoka kwa Wakala.
5. Kila mara unapotuma pesa, kumbuka kuhakiki namba ya mpokeaji kuepuka kukosea na usumbufu.
6. Hakikisha unahifadhi namba yako ya siri (PIN), simu yako na laini yako kwa usalama. Usimpe (PIN, Simu, laini yako) wala kumtajia mtu yoyote namba yako ya siri, iwe Wakala wa Tigo Pesa, mfanyakazi wa Tigo au mhudumu wa Tigo Huduma kwa wateja. Pia kumbuka kubadili namba yako ya siri mara kwa mara.
7. Tigo itakupigia kwa 100 Tu.
8. Kutoa taarifa yoyote dhidi ya udanganyifu Piga simu namba 100 au tuma ujumbe kwenda namba 15040 au barua pepe kwenda customercare@tigo.co.tz
9. Unaweza kupokea pesa kutoka nchi zaidi ya 200 duniani, na unaweza kutuma pesa kwenda nchi zote za Mashariki na Kusini mwa Afrika .
10. Kupata vigezo na masharti ya kutumia Tigo Pesa, tembelea duka la Tigo lililopo karibu nawe au www.tigo.co.tz

Unaweza kurudisha **muamala uliokosea**, **token ya luku, ku-unbar akaunti yako ya Tigo Pesa** na **kuriseti PIN**

Piga ***150*01#** chagua **6 (Jihudumie)** kisha chagua huduma unayotaka

tigo pesa

App yenye urahisi wa kushangaza!




**Fanya malipo ya Serikali**

Pakua kwenye

Google Play | App Store

tigo pesa

Kuwasaliana na huduma kwa wateja,
Piga **100** bure au tembelea duka lolote la Tigo!
Ada hizi ni kuanzia 01 Julai 2023

www.tigo.co.tz

tigo

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania wachangamkie fursa maduka fedha kigeni

**BENKI** Kuu ya Tanzania (BoT), juzi ilitoa kanuni mpya za maduka ya kubadilisha fedha za kigeni ambazo zimegawanyika katika madaraja matatu ya leseni. Katika kanuni hizo, kiwango cha juu cha mtaji wa kuanzisha biashara ya kubadilisha fedha kitakuwa Sh. bilioni moja.

Aidha, kanuni hizo zinatoa ahueni kwenye mtaji kwa wazawa huku zikipunguza ada ya leseni kwa mwaka kutoka Sh. milioni moja hadi 500,000 huku ada ya maombi ikibaki Sh. milioni moja kama ilivyokuwa katika kanuni za mwaka 2019.

Kutokana na kanuni hizo ambazo zilitolewa kwenye taarifa ya Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, duka la kubadilisha fedha za kigeni daraja A, litakalomilikiwa na mgeni au mzawa litaruhusiwa kufungua matawi sehemu yoyote ndani ya Tanzania. Lakini faraja kubwa ni kwamba wazawa wamepewa kipaumbele katika uendeshaji wa biashara za kubadili fedha kwa kupunguziwa kiasi cha mtaji tofauti na wageni. Mzawa atatakiwa kuwa na mtaji wa Sh. milioni 500 ilhali mgeni atatakiwa kuwa na Sh. bilioni moja ya mtaji.

Sambamba na hilo, duka la daraja A litaruhusiwa kufanya miamala ya papo kwa papo, kutuma fedha na kufanya biashara kama wakala wa benki, taasisi ya fedha, kampuni ya bima, huduma za fedha kwa njia ya simu, au huduma nyingine zozote za fedha kama itakavyoidhinishwa na BoT.

Kwa duka la daraja B, hili litamilikiwa na wazawa na halitaruhusiwa kufungua matawi ya kufanya biashara ya kubadilisha fedha za kigeni na sharti la mtaji ni kuwa na Sh. milioni 200. Pia linaruhusiwa kufanya miamala ya papo kwa papo na kufanya biashara kama wakala wa benki, taasisi ya fedha, kampuni ya bima, huduma za fedha kwa njia ya simu, au huduma nyingine zozote za fedha kama itakavyoidhinishwa na BoT.

Ili kufanikisha azma hiyo ya kufanyabiashara ya kubadili fedha, mwombaji anapaswa kuandika barua ya maombi BoT na kama ni kampuni inapaswa kuwa na majina ya wakurugenzi wasiopungua wawili.

Kanuni za duka daraja C litaanzishwa na hoteli yenye hadhi ya nyota tatu au zaidi kwa ajili ya kufanya miamala ya papo kwa papo kwa wateja wa hoteli pekee na leseni yake itatolewa kwa hoteli au mmiliki wa hoteli. Faida kubwa anayoipata mmiliki wa duka hilo ni kutokuwa na mtaji wa kufanya biashara hiyo.

Hatua ya BoT kuruhusu wafanyabiashara kufungua maduka ya kubadilisha fedha katika madaraja tofauti ni fursa nyingine kwa Watanzania ya kufanya uwekezaji na biashara ambayo italeta tija kwa wahusika na taifa kwa ujumla.


Licha ya tija hiyo, ni dhahiri kwamba biashara hiyo sasa itapunguza au kumaliza tatizo la uhaba wa fedha za kigeni kama ambavyo imekuwa ikilalamikiwa na Watanzania wanaofanya biashara husus an uagizaji wa bidhaa nje ya nchi. Pia biashara hiyo ni fursa nyingine ya kusaidia kutatua ukosefu wa ajira kwa vijana ambao umekuwa ukiongezeka kila mwaka.

Ni vyema Watanzania wenye nia na uwezo wa kufanya biashara hiyo wakachangamkia fursa hiyo kwa kutuma maombi kwa mujibu wa masharti yaliyotolewa ili kushiriki katika kujenga uchumi binafsi na wa nchi kwa ujumla.

Pamoja na kutolewa kwa fursa hiyo, ni vyema wafanyabiashara wakatanguliza mbele uaminifu kwa kufanya biashara hiyo kwa weledi badala ya kujiingiza katika vitendo vya uhalifu kama vile kuficha fedha na utakatishaji wa fedha.

Wakati wa uongozi wa serikali ya awamu ya tano, serikali ilifunga maduka ya kubadilisha fedha za kigeni kutokana na sababu mbalimbali. Kwa mantiki hiyo, ni vyema watakaoanzisha biashara hiyo wakajifunza hatua zilizochukuliwa na serikali ili nao wasiingie kwenye mtego huo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Na Tuntule Swebe

# Tusichezee macho tunaweza kupofuka

**IDADI** kubwa ya watu zama hizi wanasumbuliwa na matatizo ya macho, kuanzia wazee, watoto hata vijana.

Ziko shida za mtoto wa jicho, uoni hafifu, presha ya macho lakini pia kuna mambo mengine yanayohusishwa na uoni hafifu na matumizi mabaya ya macho.

Mathalani, kuna baadhi ya wanafunzi wanaosoma hata wakitembea juani wanatembea na maswali na majibu kwenye karatasi nyeupe, wakipitia kujikumbusha hata wakiwa barabarani kwenye jua kali.

Wengine hata ndani ya vyombo vya usafiri wanaendelea kujisomea nyakati za usiku wakitumia mwanga wa tochi za simu.

Lakini kwenye mwanga mkali ndipo kuna hatari . Hawafahamu kuwa hicho wanachokifanya ni hatari kwa macho yao.

Inaelezwa kuwa unaposoma juani tena kwenye karatasi nyeupe mwanga wa jua una madhara kwani mionzi inapopiga kwenye karatasi na kuakisiwa na macho yako unajiweka hatarini.

Hivyo ni vyema wanafunzi waache kusoma vitabu ni karatasi zenye mambo mbalimbali juani, hata vijana nao kusoma au kuperuzi simu siyo jambo jema, waepuke ili kuepusha madhara ya macho.

Athari wanazoweza kukutana nazo ni pamoja na kutoa machozi, kuwashwa, kuchoma choma, kuona giza na kusumbuliwa na uono hafifu.

Tatizo la macho wakati mwingine huwapata hata wale wanaopenda kutazama runinga ision wakiwa karibu ili kutaka kusikia au kupata uhondo wa kinachoonyeshwa.

Ni wajibu wa wazazi na walezi kuwasaidia watoto kwani hawatambui kuwa runinga zina miale na mionzi ambayo wanapoisogelea kwa ukaribu wanaweza kupata athari machoni,

Ni jukumu lao kuweka runinga mbali ili wanapoitazama isiweletee madhara.

Aidha, lishe duni nayo ni changamoto.Kwa upande wa vyakula hapo ndipo tatizo lilipo kutokana na kutumia lishe duni,kwa vile wengi hupendelea kula chips, mihogo ya kukaanga, chapati na vyakula vya kudokoa hapa na pale lakini si mlo kamili.

Ikumbukwe nguvu ya macho pia iko kwenye mlo hasa mboga na vyakula vya rangi ya njano kuanzia karoti, binzari, mboga za majani, mapapai, maembe na mayai.

Vijana na familia nyingi zinasahau umuhimu wa vyakula asilia kuwa vina ulinzi kwenye afya ya macho hasa vile vyenye vitamin A.

Ni vyema pia kutambua kuwa kutokomeza maradhi ya macho kunahitaji usafi ikiwamo kunawa uso na kujifuta vumbi na kunawa kwa maji safi mara kwa mara nalo ni jambo muhimu ili kujiepusha na magonjwa kama vikope.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS) watu waliosumbuliwa na maradhi ya macho kwa kutozingatia mlo kamili mwaka 2014 walikuwa 2,285.

Aidha idadi ya waliokuwa na matatizo ya macho inazidi kuongezeka na kwamba waliopata madhara ya mwanga wa jua mwaka 2020 walifikia milioni 1.5,

Hiyo hunda ni sehemu ndogo ya idadi kubwa ya Watanzania wenye shida ya kuona kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za kujisababishia kama kupuuza lishe bora, kutozingatia usafi na matumizi mabaya ya macho.

Tatizo hili linaathiri jamii kubwa hivyo kuna haja ya juhudi zaidi za kuelimisha umma kufahamu na kuzingatia kuwa Tanzania bila maradhi ya macho inawezekana.

Zipo juhudi nyingi zinazofanywa na serikali na wadau kutatua tatizo hili kwa kuhakikisha wataalamu na madaktari hupita sehemu mbalimbali ili kuhudumia watu waliopata madhara au maradhi ya macho.

Hata hivyo, kuna haja ya kuongeza zaidi kampeni ili wataalamu wawafikie watu wengi zaidi walioko sehemu mbalimbali kuanzia shuleni, vyuoni, nyumba za ibada, ofisini, kwenye minada, masoko mijini na vijijini ili kutoa ujumbe na elimu zaidi.

Wataalamu wa lishe nao washirikiane na jamii kuainisha aina mbalimbali za vyakula vinavyyongeza uwezo wa macho na taatifa ziwafikie walimu shuleni, wazazi na walezi kliniki, wananchi vijijini na ili kutumia mlo unaowaepusha na magonjwa ya macho.

## Serikali yahimiza nguvu uchumi kidijitali kwa wanawake, vijana

**Na Mwandishi Wetu**

KWA kuwa wanawake na vijana ni msingi na chachu ya mabadiliko ya masuala yote ya kiuchumi na kijamii, serikali imetaka wadau wote kushirikiana kuwezesha makundi hayo kuchangamkia fursa zinazoambatana na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Aidha imesisitizwa kundi hilo lenye nafasi ya kipekee katika kuelimisha umma teknolojia mpya za kidijitali, matumizi salama na yenye tija ya TEHAMA ili kuwesha uchumi wa kidijitali ulio shirikishi, "inclusive digital economy" ni lazima liandaliwe kuwa na kasi ya matumizi ya teknolojia za kidijitali.

Kauli hizo zimetolewa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Selestine Kakele, wakati akifungua mkutano wa wanawake kwenye kongamano la saba la TEHAMA jana lililoandaliwa na Tume ya TEHAMA chini ya uongozi wa Dk. Nkundwe Mwasaga.

"Serikali, kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inapenda kuwashukuru wadau wote wa maendeleo ya TEHAMA katika kulitambua kundi hili muhimu na kuendelea kuwezesha wanawake na vijana kuchangamkia fursa zinazoambatana na TEHAMA," alisema.

Alisema serikali imeweka mazingira rafiki ya kukuza na kuibua ubunifu, kuchochea uwekezaji na uendelezaji wa Teknolojia za kisasa na TEHEMA kwa kutunga na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, kanuni na taratibu pamoja na miongozo mbalimbali.

Aidha, alisema nguzo ya uchumi jumuishi wa kidigitali, inakusudia kupunguza na hatimaye kuondoa kabisa pengo baina ya watu wanaofikia na kutumia huduma za kidigitali na wasiopata fursa hiyo (digital divide). Aidha, nguzo hii inaweka msingi wa kushughulikia vikwazo vya kupata fursa ya kupata elimu na mafunzo ya TEHAMA kwa jamii. Lengo ni kuhakikisha kwamba kila mtu pasipokujali hali yake au sehemu anayotoka anashiriki na kufaidika na uchumi wa kidijitali.

Alitoa rai kwa wanawake kutumia jukwaa hilo na fursa hiyo, kupaza sauti zao na kupitia sauti hizo kama taifa kujadiliana vikwazo vinavyowakabili wanawake na kufanya washindwe kuchangamkia matumizi ya teknolojia na TEHAMA kwa ujumla katika shughuli zao za kila siku.

Aidha katika matumizi hayo alisema kwamba wanawake na vijana wana nafasi maalumu ya kuongoza harakati za kupinga matumizi mabaya ya TEHAMA.

Nguzo ya uchumi jumuishi wa kidijitali, inakusudia kupunguza na hatimaye kuondoa pengo baina ya watu wanaofikia na kutumia huduma za kidijitali na wasiopata fursa hiyo (digital divide). Aidha, nguzo hiyo inaweka msingi wa kushughulikia vikwazo vya kupata fursa ya kupata elimu na mafunzo ya TEHAMA kwa jamii. Lengo ni kuhakikisha kwamba kila mtu pasipokujali hali yake au sehemu anayotoka anashiriki na kufaidika na uchumi wa kidigitali.

"Wakati tukiendelea kuweka mazingira mazuri kwa ukuaji wa TEHAMA nchini, ni vema tukashirikiana pamoja kutatua changamoto zinajitokeza kwa wakati. Tuhakikishe tunatoa elimu kwa umma juu ya matumizi salama ya TEHAMA pamoja na kujikinga na matumizi mabaya ya TEHAMA ili kujipatia maendeleo," alisema.



Naibu Katibu Mkuu wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Selestine Kakele (katikati), akifuatilia mada katika siku ya kwanza ya kongamano la TEHAMA. Anayefuatia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Tume ya TEHAMA, Profesa Leonard Mselle na Mkurugenzi Mkuu wa Tume hiyo, Dk. Nkundwe Mwasaga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Temeke kumchukulia hatua Katibu CWT

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Japhet Maganga, akiendelea kutorejea kwenye kituo chake cha kazi tangu alipotakiwa kufanya hivyo, Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imeanza mchakato wa kufungua shauri la kinidhamu.

Akizungumza na Nipashe Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Elihuruma Mabelya, alisema Maganga ni mtumishi wa Temeke na alitakiwa kuripoti kazini Oktoba Mosi, mwaka huu kama alivyotakiwa katika tangazo la wito lakini hadi sasa hajaripoti.

"Hatujawahi kumwona tunaendelea na utaratibu wetu wa ndani, sisi tunajua ni mfanyakazi wa Temeke kinachofanyika ni kuchukua hatua za kinidhamu... Mchakato wa kufungua shauri la kinidhamu unaendelea."

"Yule ni mtumishi wa serikali hapaswi kuigomea serikali sisi tunachojua yeye ni mtumishi wetu kule aliko kibali kimeisha sio tena sehemu yake ya kazi," alisema.

Oktoba 3, 2023, Mkurugenzi huyo alisema kama Maganga hatarejea baada ya siku saba tangu alipotakiwa kufanya hivyo, atafunguliwa shauri la nidhamu.

Wakati uongozi wa manispaa hiyo ukitoa kauli hiyo, Rais wa CWT, Leah Ulaya, alisema bado hawajapokea barua ya kumtaka Maganga kurejea katika kituo chake cha kazi na anaendelea na majukumu yake ya Ukatibu wa CWT.

"Kwanza sijajua ile nyaraka iliyoonekana ilikuwa ni barua au tangazo kwasababu ili hatua zozote zichukuliwe ni lazima kuwe na mchakato halali ili kufanyia kazi."

"Suala la kibali ni mwajiri na mwajiriwa wake, na atamjulisha kwamba nakubali uendelee au sikubali sasa mwajiriwa hajapata na wala sisi hatuna nakala kwa hiyo hatuwezi kufanya hatua zozote na sisi hatuna chochote tunachojua zaidi ya kujua kwamba ni Katibu Mkuu ataendelea kuwapo na kazi zinaendelea," alisema.

Alipotafutwa Maganga ili kujua sababu za kutorejea kituo chake cha kazi, mwandishi alipojitambulisha alijibu "Nipo kwenye kikao" na kukata simu.

Septemba 25, 2023 siku ya kikao cha baraza la dharura la CWT jijini Dodoma, Nipashe ilimtafuta Maganga kuhusu suala hilo, na kujibu kuwa bado hajapewa barua ya kukataliwa kwa ombi lake la kuendelea kuazimwa na chama hicho."Sijapata barua nikipata nitazungumza, lakini kwa sasa sina cha kuzungumza."

Septemba 23, 2023, Mkurugenzi Mabelya alitoa tangazo akimtaka Maganga kurejea kwa mwajiri wake ifikapo Oktoba mosi, mwaka huu, baada ya serikali kutokubali maombi ya kuendelea kuazimwa na CWT.

Katika tangazo hilo, inaonesha Maganga aliomba na kibali cha kuazimwa na CWT Agosti 2017 kilichomalizika Septemba 30, 2020.

Tangazo hilo linasema Maganga ambaye cheo chake ni mwalimu mwandamizi, aliomba tena kibali cha kuazimwa kwa mara ya tatu lakini Katibu Mkuu Utumishi hakuridhia maombi hayo.

"Hivyo basi Mwalimu Japhet Maganga anapaswa kurejea kwenye kituo chake cha kazi mara moja Oktoba mosi, 2023," lilisema tangazo hilo.


Maganga alichaguliwa Desemba mwaka jana na Mkutano Mkuu wa CWT kuwa Katibu Mkuu kuchukua nafasi ya Deus Seif ambayo awali alikuwa akitumikia nafasi ya Naibu Katibu Mkuu.

Januari 25, mwaka huu, Maganga, Makamu wa Rais wa CWT, Dinna Mathaman na Rais wa CWT, Leah Ulaya waliteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan kuwa wakuu wa wilaya, lakini ni Dinna pekee alikwenda kuapa kushika nafasi ya ukuu wa Wilaya ya Uvinza mkoani Kigoma.

Leah aliteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe mkoani Geita wakati Maganga akiteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kyerwa, mkoani Kagera hawakwenda kuapa katika nafasi hiyo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Mbunge ashtushwa kituo cha afya kuanza kubomoka kabla hakijatumika

Na Neema Emmanuel

BAADA ya gazeti hili kuripoti zahanati mbili zilizojengwa kwa nguvu za wananchi kushindwa kutoa huduma licha ya kukamilika kwa zaidi ya miaka minne, huko wilayani Maswa mkoani Simiyu, kituo cha afya kingine kimebainika kuanza kubomoka kabla ya kuanza kutumika.

Kituo cha Afya cha Miswaki, kilichopo Kata ya Mwasubuya, wilayani Bariadi mkoani hapa kilichogharimu zaidi ya Sh. milioni 500, kinadaiwa kujengwa chini ya kiwango huku baadhi ya maeneo yakianza kubomoka kabla ya kuanza kutumika.

Ubovu wa kituo hicho ulibainika juzi katika ziara ya Mbunge wa Jimbo la Bariadi, Mhandisi Kundo Mathew, alipotembelea na kufanya ukaguzi na kueleza kutoridhishwa na ujenzi wake.

"Huu mradi bado haujaanza kazi, lakini akija mtu hapa atadhani mradi huu ulishaanza kufanya kazi siku nyingi na kutelekezwa kama pagale, viongozi mmeuona baada ya kukagua hatua kwa hatua na tumejiridhisha huu mradi upo chini ya kiwango," alisema mbunge huyo ambaye ni Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Aidha, alisema kituo hicho kinachotarajiwa kutoa huduma kwa wananchi, kimeanza kushambuliwa na mchwa katika kenchi za paa na muda si mrefu zinaweza kuanza kushuka na kwamba eneo hilo si salama kwa wagonjwa.

Alisema ofisi ya mbunge itaandika barua kwa ofisi ya Mkurugenzi kumwelekeza ampe taarifa mhandisi wake awarejeshe mafundi wafanye marekebisho mahali palipo na kasoro.

Pia hatua inayofuata ni kufanya ukaguzi wa miradi yote ndani ya jimbo lake na ataomba nyaraka zote zikiwamo za ununuzi na katika suala hilo ataiomba ofisi ya TAKUKURU wampe mtu mmoja ambaye atakuwa akizunguka naye, kwa kuwa wamebaini mabafu mengi na vyoo hayana vigae, hakuna mabomba ya plastiki huku vigae vingine vikiwa vimekatika na ujenzi ukiwa chini ya kiwango.

"Hatuwezi kukaa kimya kwa vitu kama hivi fedha zimetolewa na kilichofanyika hakionekani rangi yenyewe iliyopigwa inamwaga unga wa chokaa ukiigusa na fundi anadai kazi yake tayari kamaliza haiwezekani," alisema mbunge huyo.

Diwani wa Kata ya Mwasubuya, Sylvester Chenge, akizungumzia suala hilo alisema wananchi wa eneo hilo walikuwa na mategemeo ya kupata huduma katika kituo hicho na kuwapunguzia adha ya kufuata huduma hiyo mbali, lakini ujenzi wake unakatisha tamaa ya kupata huduma husika.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu CCM Mkoa wa Simiyu, Kitebo Masanja, alisema mradi huo upo chini ya kiwango na haujasimamiwa ipasavyo na kutoa mfano wa vigae ambavyo vilivyowekwa kuwa na mabonde na kuwaomba viongozi wa serikali hususan mkuu wa wilaya kusimamia shughuli hizo za kimaendeleo kwa kutembelea maeneo ya miradi waone zinavyofanyika. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi, Halid Mbwana, alipoulizwa kuhusu suala hilo hakuwa tayari kutoa ufafanuzi badala yake alimshauri mbunge huyo kujenga utaratibu wa kuongozana na wataalamu ili waweze kujibu hoja wakati wa ukaguzi wa miradi.

Katika ukaguzi wa jengo la kituo hicho, ilibainika milango kuanza kuharibiwa huku sehemu nyingine zikionesha kubomoka kinyume na matarajio.

Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ya 2021/22 ilithibitisha uwapo wa miradi iliyotelekezwa na makandarasi yenye thamani ya Sh. bilioni 3.86 katika mikoa ya Rukwa, Simiyu, Arusha, Shinyanga, Kigoma, Manyara na Tarime.

Aidha, utelekezwaji wa miradi hiyo unaelezwa kuchangiwa na ufinyu wa bajeti, usimamizi duni na upungufu wa kitaalamu katika usimamizi.

Ripoti hiyo ilieleza kutokamilishwa kwa miradi hiyo kunainyima jamii kunufaika na miradi husika kama ilivyolengwa.

Aidha, kutotekeleza miradi kunaweza kusababisha gharama kubwa ya kuikamilisha na kuhatarisha uamuzi wa baadaye wa utoaji wa fedha na mgawo wa rasilimali.

Ushauri uliotolewa na CAG kwa uongozi wa wakala ni kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ili kufuatilia maendeleo ya miradi na kubaini masuala yoyote yanayoweza kujitokeza kuwezesha hatua za marekebisho kuchukuliwa kwa wakati na kushughulikia masuala yoyote kabla hayajatokea.

Licha ya ushauri huo ambao ulielekezwa pia kwa Mkoa wa Simiyu unaonekana kutokufuatwa kutokana na miradi mbalimbali kuendelea kutelekezwa huku mingine ikijengwa chini ya kiwango na kuthibitisha kutokufanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara.

Kanuni ya 114 (b), (c), na (d) ya ununuzi wa umma, 2013 inaitaka taasisi kusimamia ununuzi wa bidhaa, huduma au kazi yoyote inayofanywa na itafuatilia maendeleo na ukamilishaji wa kazi kwa wakati kwa mujibu wa masharti ya kila mkataba.

Kadhalika, inataka kuchukua au kuanzisha hatua za kurekebisha au kuadhibu ukiukwaji wa masharti ya mkataba na kuhakikisha kwamba majukumu yaliyowekwa na mkataba yanatekelezwa kikamilifu.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Jerry Silaa (wa pili kulia), akiangalia ramani na baadhi ya wataalamu wa sekta ya ardhi katika ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Singida juzi. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

## Viongozi TANAPA watakiwa kuongeza watalii, mapato

Na Mwandishi Wetu

SHIRIKA la Hifadhi za Taifa Nchini (TANAPA), limewataka viongozi wake kuongeza idadi ya watalii wa ndani na wa kutoka nje ya nchi wanaokwenda kutembelea vivutio mbalimbali katika hifadhi zake ili kuongeza mapato ya serikali.

Rai hiyo imetolewa na Kaimu Kamishna wa TANAPA, Juma Kuji, katika hafla ya kuwavisha vyeo makamishna wasaidizi waandamizi wapya wanane iliyofanyika katika ofisi za makao makuu ya mamlaka hiyo mjini hapa mwishoni mwa wiki iliyopita.

Kuji alifafanua kuwa ametoa rai hiyo ya kuongeza idadi ya watalii kwa viongozi hao kutoka ndani na nje ya nchi wanaokwenda kutembelea vivutio hivyo na kuiwezesha TANAPA kutimiza kusudi na kasi ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema ili waweze kuendena na kasi hiyo, viongozi hao wanatakiwa kuelekeza nguvu zao katika kusimamia majukumu yao kama serikali inavyotaka ili kutimiza lengo lake la kuhakikisha sekta hiyo inaongeza mapato zaidi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na matumizi mengine.

Kuji aliwataka makamishna hao waliopandishwa vyeo kufanya kazi kwa bidii mchana na usiku ili kuiletea mamlaka hiyo heshima Tanzania kwa mataifa mbalimbali duniani.

Alisema angependa kuona makamishna hao kutoka vitengo mbalimbali vya TANAPA wanafanya kazi kwa weledi mkubwa na kwa mfumo wa mamlaka hiyo na kuwa mfano mzuri ndani na nje ya mipaka ya Tanzania.

"Nimewapandisha vyeo, sasa nataka mkafanye kazi kwa bidii na kwa kufuata taratibu zilizopo ndani ya Jeshi letu la TANAPA," alisema Kuji na kusisitiza kuwa:

"Nataka pia muwe viongozi wazuri katika maeneo mnayokwenda kuyasimamia na kuwa mfano bora kwa askari na maofisa mtakaowaongoza."

Amewapongeza makamisha hao kwa kuwa wavumilivu na kuonyesha jitihada za kuhakikisha jeshi lililopo ndani ya mamlaka hiyo linaendelea kufanya vizuri ndani na nje ya Tanzania kwa kulinda na kusimamia rasilimali za Taifa kwa manufaa ya sasa na kwa vizazi vijavyo.

# Watoto 37 wafanyiwa upasuaji wa moyo

Na Christina Mwakangale

TAASISI ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI) imewafanyia upasuaji wa moyo watoto 37 akiwamo mchanga mwenye umri wa mwezi mmoja, aliyezaliwa akiwa na matatizo manne katika moyo.

Matatizo katika moyo wa mtoto huyo yanajumuisha mshipa unaotakiwa kujifunga mara tu mtoto anapozaliwa, kutojifunga.

Kambi ya siku tano iliyofanyika katika taasisi hiyo, imeokoa Sh. milioni 950 ambazo iwapo zingetumia kwa watoto hao kwenda nje ya nchi kwa ajili ya matibabu hayo.

Bingwa wa Upasuaji wa Moyo kwa Watoto kutoka JKCI, Dk. Godwin Sharau, alibainisha hayo ilipohitimishwa kambi hiyo maalum ya siku tano juzi jijini Dar es Salaam, ikifanywa na wataalamu wa JKCI kwa kushirikiana na wenzao kutoka Shirika la Mending Kids la Marekani.

Bingwa huyo alisema watoto 16 walifanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo wa kuziba matundu, kurekebisha valvu za moyo na mishipa ya damu ambayo haikuwa sawa. Kama wangepelekwa nje ya nchi kwa ajili ya matibabu, gharama ingekuwa Sh. milioni 250.

"Matibabu haya kwa kundi la kwanza kwa watoto 16 kufanyika JKCI yamegharimu Sh. milioni 90 na baadhi ya watoto wamepatiwa msamaha wa matibabu kutokana na hali zao za kiuchumi kutomudu gharama za matibabu.

Alifafanua kwamba mwaka huu ni wa 10 tangu taasisi hiyo ianze kushirikiana na shirika hilo. Ushirikiano umezaa matunda na kila mwaka wataalamu wa shirika hilo hufika JKCI na mbinu mpya za matibabu na kutoa vifaa vya matibabu kwa watoto bila gharama.

Bingwa wa Magonjwa ya Moyo kwa Watoto kutoka taasisi hiyo, Dk. Stella Mongela alisema upasuaji wa tundu dogo kwa kutumia mtambo wa Cathlab, umefanyika kwa watoto 21 waliokuwa na magonjwa ya moyo ya kuzaliwa nayo, kama matundu na mishipa ya damu iliyobana.

Alisema matibabu ya upasuaji mdogo wa moyo kwa watoto hao, yamegharimu chini ya Sh. milioni 100 kwa kufanyika nchini. Kama wangepelekwa nje ya nchi matibabu yao yangefika Sh. milioni 700.

Bingwa wa Upasuaji wa Tundu Dogo kwa kutumia mtambo wa Cathlab kwa Watoto kutoka Shirika la Mending Kids, Dk. Darren Berman, alisema madaktari kutoka shirika hilo wataendelea kushirikiana na madaktari wa JKCI.

Alisema utaalamu wa kutoa huduma za upasuaji wa moyo kwa watoto JKCI umeongezeka, hivyo sasa hakuna haja ya watoto wa Watanzania wenye magonjwa ya moyo kupelekwa nje ya nchi.

Prisca Elius, mmoja wa wazazi ambaye mwanawe amefanyiwa matibabu, aliishukuru taasisi hiyo, akisema awali alipoteza matumaini kwa kuwa hakujua ni kwa namna gani angefika kambi hiyo na kupata fedha kwa ajili ya matibabu.

# TANGAZO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**
**(IDA CREDIT NO. 7215-TA)**

## TANGAZO KWA UMMA

## ZOEZI LA ULIPAJI FIDIA KWA WATU WANAOATHIRIKA NA MRADI

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inatekeleza mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kwa lengo la kukabiliana na mafuriko na kuboresha matumizi ya ardhi katika eneo la chini la bonde. Ili kufanikisha utekelezaji wa mradi, Serikali inatarajia kuwahamisha watu wote wanaoathirika na mradi kwa kuwalipa fidia ya mali zao zinazoathirika.

Mthamini Mkuu wa Serikali ameshaidhinisha jedwali la fidia lililozingatia maoni yake na wadau wengine, na sasa zoezi la ulipaji fidia linatarajiwa kuanza mapema iwezekanavyo. Ikumbukwe kuwa jedwali hili la fidia linawahusu waathirika wa mradi walioafiki fidia zao wakati wa zoezi la kuhakiki fidia lililofanyika mwezi Machi 2023.

Kampuni ya kusimamia ulipaji wa fidia (PROPERTY MATRIX LIMITED), inayofanya kazi kwa niaba ya OR-TAMISEMI, inatarajia kufanya zoezi la kusainisha mikataba ya malipo ya fidia pamoja na kuhakiki taarifa za benki kabla ya kufanya malipo. Kampuni hii itafanya zoezi hili katika kila Kata kwa ratiba ifuatayo:

| Eneo la Usainishwaji | Kata | Mitaa Inayohusika | Tarehe |
|---|---|---|---|
| Ukumbi wa DRIMP (Ilala Kota) | Mchikichini | Msimbazi Bondeni | 18 hadi 20/10/2023 |
| | | Misheni Kota | 21 na 22/10/2023 |
| | | Ilala Kota | |
| | Kariakoo | Kariakoo Kasikazini | |
| | Upanga Magharibi | Charambe | 31/10/2023 hadi 02/11/2023 |
| | Jangwani | Mtambani A | |
| | | Mtambani B | |
| | | Jangwani | |
| Ofisi ya Kata - Magomeni | Magomeni | Suna | 23 hadi 25/10/2023 |
| Ofisi ya Kata - Mzimuni | Mzimuni | Idrisa | 26/10/2023 |
| | | Mtambani | |
| | | Mwinyi Mkuu | |
| Shule ya Msingi Mapinduzi - Kigogo | Kigogo | Kigogo Mbuyuni | 27 na 28/10/2023 |
| | Hananasif | Mkunguni A | 29 na 30/10/2023 |
| | | Mkunguni B | |
| | | Hananasif | |
| Ukumbi wa DRIMP (Ilala Kota) | | Kawawa | 3 hadi 5/11/2-23 |

Wahusika wanaombwa kufika katika maeneo ya usainishwaji wakiwa na vitambulisho (NIDA/Uchaguzi) na nyaraka zote zinazowathibitisha iwapo wanapokea malipo kwa niaba.

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MRADI WA UENDELEZAJI WA BONDE LA MSIMBAZI**
**(IDA CREDIT NO. 7215-TA)**

## TANGAZO KWA UMMA

## ZOEZI LA UHAKIKI WA MALI ZILIZOATHIRIKA NA MRADI KWA WATU AMBAO HAWAKUAFIKI VIWANGO VYA FIDIA NA WALIOSAJILI MALALAMIKO


Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inatekeleza mradi wa uendelezaji wa Bonde la Msimbazi kwa lengo la kukabiliana na mafuriko na kuboresha matumizi ya ardhi katika eneo la chini la bonde. Ili kufanikisha utekelezaji wa mradi, Serikali inatarajia kuwahamisha watu wote wanaoathirika na mradi kwa kuwalipa fidia ya mali zao zinazoathirika.

Kufuatia zoezi la uhakiki wa fidia lililofanyika mwezi Machi 2023, baadhi ya waathirika wa mradi hawakuafiki viwango vya fidia walivyo onyeshwa, na baadhi walisaini kuridhia viwango vya fidia na kisha kuandika barua za malalamiko. Katika kushughulikia malalamiko yao, OR-TAMISEMI inatarajia kufanya zoezi la kuhakiki upya mali za waathirika hao kwa kuzingatia aina ya malalamiko yao. Kutakuwa na timu mbili za wathamini kwa wilaya za Kinondoni na Ilala ambazo zitapita kwenye makazi ya waathirika husika kwa ratiba ifuatayo:

| Tarehe | Mtaa Itakayotembelewa | |
|---|---|---|
| | Timu ya Ilala | Timu ya Kinondoni |
| 19 na 20/10/2023 | Msimbazi Bondeni | Kigogo Mbuyuni |
| 23 na 24/10/2023 | Charambe | Hananasif |
| | Ilala Kota | Mkunguni A |
| | Mtambani A | Mkunguni B |
| | Mtambani B | Idrisa |
| | Kariakoo Kaskazini | Suna |
| | | Mwinyimkuu |

Wahusika wanaombwa kutoa ushirikiano kwa kuwepo katika ofisi za Serikali za Mitaa yao kuanzia saa 2:00 asubuhi.

**KATIBU MKUU**
**OFISI YA RAIS - TAMISEMI**





# Wananchi watakiwa kujiunga na NHIF kabla ya maradhi

**Na Halima Ikunji,** TABORA

WANANCHI mkoani Tabora wameshauriwa kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), ili kurahisisha mchakato wa kupata matibabu ya haraka ambayo yanatolewa na mfuko huo nchini.

Hayo yalibainishwa juzi na Meneja wa NHIF mkoani hapa, Salum Adam, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ufafanuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu mfuko huo.

Alisema kuwa wananchi wanapaswa kujiunga na mfuko huo kabla ya kuugua ili iliwe rahisi kupata huduma ya matibabu yanayotolewa katika hospitali mbalimbali nchini.

"Ipo tabia ya watu kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya wanapoanza kuugua jambo ambalo sio nzuri na hali hiyo inasababisha kukosa matibabu ya haraka mpaka mchakato utakapokamilika," alisema Adam.

Alisema kwamba iwapo mfuko huo ungekuwa unatoa huduma za aina hiyo utafilisika na utashindwa kutoa huduma kama ilivyokusudiwa na malengo ya serikali ya kutoa huduma za afya kwa wananchi wake yatakufa.

Meneja huyo alisema NHIF mkoani hapa hauna changamoto ya ucheweleshaji wa vitambulisho isipokuwa kuna tatizo la kimazingira na mfumo wa uwasilishaji wa kadi kwa wananchi kupitia halmashauri zao.

Alisema kwamba mchakato wa kuwafikishia kadi wanachama ambao wengi ni watumishi wa serikali umekuwa ukifanyika kupitia halmashauri na hivyo muda wa kupata kadi unategemea umbali anaokaa mwanachama.

Alisema: "Mtumishi akijaza fomu ya bima kwanza anaipeleka halamashauri kisha halmashauri inaipeleka fomu NHIF na baada ya mchakato wa kadi NHIF hurudisha tena halmashauri mchakato ambao unaweza kuchelewa kadi kufika kwa mwanachama anayeishi mbali".



Katibu Mkuu wa Chama cha ACT- Wazalendo, Ado Shaibu (wa pili kulia mbele) akiwa na viongozi wenzake wakienda kwenye mkutano ulioandaliwa na uongozi wa Kata ya Azimio wilayani Temeke Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA**

# Wafugaji wapongezwa kurejesha mkopo kwa wakati

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

OFISA Maendeleo ya Jamii wilayani Kishapu, Abednego Madole, amekipongeza kikundi cha wafugaji cha umoja ni nguvu kilichopo katika Kijiji cha Beledi kwa kufanikiwa kurejesha mkopo wa Sh.milioni 4.3 ambao walipatiwa na halmashauri.

Alitoa pongezi hizo juzi wakati wa halfa ya kukabidhi ng'ombe wengine kwa wanakikundi hao.

Madole alisema kikundi hicho ni mfano wa kuigwa kwa sababu baadhi ya vikundi ambavyo vimepewa mkopo na halmashauri vimekuwa vikisuasua kurejesha marejesho na kufikia hatua ya kupelekana mahakamani.

"Hongereni sana wanakikundi kwa hatua mliyofikia mmekuwa mfano kwa vikundi vingine, jambo la kumaliza kurejesha mkopo ni jambo kubwa sana, hii inaonyesha ni jinsi gani mlivyo na uwezo wa kujisimamia, Halmashauri ipo tayari kuendelea kushirikiana na nyie kupitia Ofisi ya Maendeleo ya Jamii," alisema.

Katibu wa kikundi hicho, Nkuba Shija Masebo, alisema kwamba kikundi kilianza na mtaji wa Sh.75,000 baada ya hapo walipata mkopo wa Sh. milioni 4.3 kutoka halmashauri ambao uliwasaidia kununua mbuzi 42 na hadi sasa kikundi kina mbuzi 192 na ng'ombe tisa.

Alisema kikundi hicho baada ya kurejesha mkopo wote sasa kimebaki na faida ya Sh.800,000 fedha ambazo watazitumia kuendelea mtaji katika kikundi chao na kuinuka kiuchumi.

# FAO, serikali wazindua kampeni ya upandaji miti ya matunda

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kwa kushirikiana na serikali, limezindua kampeni ya upandaji miti ya matunda na rafiki wa maji wilayani Kasulu mkoani Kigoma, ili kusaidia uhifadhi wa mazingira na uhakika chakula.

Kampeni hiyo ilizinduliwa mapema wiki hii wakati Tanzania ilipoungana na mataifa mengine ulimwenguni kuadhimisha Siku ya Chakula Duniani.

Wakizungumza wakati wa upandaji miti 1,000 katika Kijiji cha Kasangezi wilayani Kasulu iliyotolewa na shirika hilo, baadhi ya wananchi na viongozi wamesema kwa sasa mazingira yameathiriwa kutokana na vitendo vya ukataji wa miti onyo.

Pia, walipongeza juhudi za wadau katika kuhamasisha upandaji miti na utunzaji wa mazingira.

Ofisa Kilimo kutoka FAO, Theresia Massoy alisema dunia inakumbwa na mabadiliko ya tabia nchi, hatua ambayo inatakiwa kuungwa mkono na mashirika na serikali ili kuhifadhi mazingira.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Mbegu za Kilimo Tanzania (TARI Kihinga Kigoma), Dk. Filson Kagimbo, alisema juhudi hizo zitakuwa chachu ya kutunza mazingira.

Alisema maonesho ya Siku ya Chakula Duniani yalifanyika mkoani Kigoma kuanzia Oktoba 10 hadi 16, yaliwaleta wadau, jumuiya ya kimataifa na serikali.

Alisema kumekuwa na shughuli mbalimbali ambapo katika kilele, wakulima walizawadiwa vifaa vitakavyowasaidia katika shughuli zao za kilimo.

Aliongeza kuwa mpango huu wa pamoja ulilenga kutoa mtazamo wa mnyororo wa thamani katika kushughulikia minyororo ya thamani ya mahindi, mihogo, maharage na uzalishaji wa mifugo ili kuongeza uwekezaji wa wakulima wadogo.

Wakati huohuo, katika kusherehekea Siku ya Chakula Duniani pamoja na Siku ya Mwanamke Kijijini, UN na wadau wake wamefanya maonesho maalumu yaliolenga kuhamasisha kilimo hifadhi na mbegu asili ili kuleta tija kwenye kilimo.

Maonesho hayo yaliyofanyika mkoani Kigoma yalimalizika juzi kwa kuendesha mashindano ya ngalawa yaliyolenga kuhamasisha uvuvi salama.

Mratibu Mkazi wa UN, Zlatan Milisic, alisema maonesho hayo yamefanyika chini ya Mpango wa Pamoja wa Kigoma (KJP), awamu ya kwanza uliotekelezwa mkoani Kigoma na UN tangu 2017 ukilenga kutatua changamoto zinazoukabili mkoa huo.

# RC ataka mpango mkakati kuwawezesha vijana kiuchumi

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Martine Shigela, amewataka watendaji wa serikali kuweka mkakati maalumu wa kuwawezesha vijana mkoani hapa ili wajikwamue kiuchumi, kukuza kipato chao na pato la taifa.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akifungua mafunzo ya siku moja ya matumizi sahihi ya matokeo ya takwimu za Sensa ya Watu na Makazi yaliyotolewa na maofisa kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS).

Mkuu huyo wa mkoa alitolea mfano kuwa mji mdogo wa Katoro uliopo Halmashauri ya Geita, watoto 2,000 huzaliwa kwa kipindi cha mwezi mmoja, hivyo ipo haja ya kuwaandalia mkakati wa fursa. Katika hatua nyingine, Shigela aliwataka watendaji kutumia takwimu za matokeo ya sensa kubaini utendaji kazi kwenye sekta ya madini, kilimo, uvuvi, mifugo na hifadhi kwenye maeneo yao ili kuhakikisha wananchi wananufaika.

Alitaja matokeo hayo kuwa ni muhimu katika mipango ya maendeleo nchini, huku akimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha Sensa ya Watu na Makazi inafanyika nchi nzima na kukamilika kwa wakati kwa kutumia teknolojia ya kisasa.

Mtakwimu Mwandamizi, Mdoka Maulid kutoka NBS alisema kuwa Sensa ya Watu na Makazi ni tofauti na utafiti, hivyo takwimu zote kuanzia ngazi ya vijiji, mitaa na kata kufikia Desemba mwaka huu zitazinduliwa na kwamba mpaka sasa ripoti 11 za matokeo hayo zimeshazinduliwa.

Meneja Takwimu wa Mkoa wa Geita, Khalidi Msabaha, alisema kuwa matokeo hayo ni nyenzo muhimu katika mipango ya maendeleo na kusaidia matumizi sahihi ya takwimu hasa kwa makundi maalumu ikiwamo wazee, watoto na watu wenye ulemavu.

Mbunge wa Geita Mjini, Constantine Kanyasu, aliipongeza NBS kwa kuweka mafunzo ya Sensa ya Watu na Makazi mkoani hapa kwa ajili ya watumishi na wananchi, akisema yatasaidia kuweka mipango ya kimaendeleo kutokana na mkoa huo kukua kwa kasi.



Ukurasa 12

**MIAKA 24 KUMKUMBUKA MWALIMU**
**BBT ilivyowekeza kimkakati kumwenzi Mwalimu Nyerere**



Ukurasa 13

Uchaguzi mdogo ubunge, udiwani ulivyo muhimu kufikia maendeleo



Ukurasa 14

**VITA ISRAEL Vs PALESTINA**
**Benjamin Netanyahu akosolewa kupambana ili kujitetea kisiasa**


# siasa

JUMATANO OKTOBA 18, 2023

Nipashe

HABARI BORA NA KAMILIFU


## JICHO UCHAGUZI S/MITAA, MKUU

# Watetezi demokrasia wataka uwazi katiba mpya, mgombea huru, vyama kuungana

**Na Sabato Kasika**

NI hivi karibuni wadau wa demokrasia wanakutana Dar es Salaam kutathmini miaka 30 ya kurejeshwa mfumo wa vyama vingi vya siasa katika kusanyiko lenye wadau takribani 259 kutoka Bara na Visiwani likileta pamoja wanasiasa, asasi za kiraia na wanahabari kujadili kwa kina miongo mitatu ya mfumo huo katika kudumisha demokrasia.

Baada ya mkutano maazimio kadhaa kwa serikali yanatolewa washiriki wakiamini kuwa ikiwa yatazingatiwa uchaguzi wa serikali za mitaa na mkuu wa mwaka 2025 unaweza kuwa huru, haki na unaoaminiwa na kukubalika.

Mwenyekiti anayepewa jukumu la kusimamia ukusanyaji wa maazimio ya wadau hao ni mwanahabari mbobezi Absalom Kibanda, anayetaja azimio la kwanza kuwa ni kuitaka serikali kuweka wazi mchakato mzima wa katiba mpya ili wananchi waufahamu na kushiriki kikamilifu katika kuufanikisha.

La pili, ni serikali kufanya marekebisho ya sheria ya mabadiliko ya katiba pamoja na sheria ya kura ya maoni, huku pendekezo la tatu likiwa ni serikali na wadau wa uchaguzi kufuata na kuheshimu sheria za uchaguzi, hususan Jeshi la Polisi kutovunja sheria hizo kipindi cha uchaguzi.

"Azimio la nne ni serikali ifanye maboresho ili kuruhusu mgombea binafsi kama ilivyoamuliwa na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu katika kesi ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na ile iliyofunguliwa na Mchungaji Christopher Mtikila dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2011," anasema Kibanda.



Wadau wa demokrasia katika mkutano wa kufanikisha uchaguzi ujao. **PICHA: SABATO KASIKA**

Katika mwendelezo huo wa azimio la tano ni uchaguzi wa serikali za mitaa usimamiwe ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), na kufanya maboresho ya daftari la kudumu la wapigakura ili kukidhi matakwa na vigezo vya uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu.

"Wadau wameazimia kufanyika mabadiliko madogo ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ili kuunda tume huru ya uchaguzi na kuweka kipengele cha tume kushtakiwa mahakamani, kupinga matokeo ya urais mahakamani kama ilivyoamuliwa na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu katika kesi namba nane ya 2018 ya Jebra Kambole dhidi ya Jamhuri ya Muungano, pia vigezo vya mshindi wa nafasi ya urais iwe ni kura asilimia 51," anasema mwanahabari huyo.

Aidha, katika azimio la saba, anasema serikali iweke uwiano wa kijinsia nafasi za ngazi zote angalau kwa asilimia 40 na kwamba hilo liwe kwenye uongozi wa vyama vya siasa.

Halikadhalika, wanataka serikali iheshimu maamuzi ya Mahakama ya Afrika ya Jumuiya ya Afrika na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ili kuimarisha misingi ya demokrasia nchini na ukanda wa Afrika.

"Kutokana na hilo wadau wanatoa wito kwa serikali kutekeleza maamuzi ya mahakama za kikanda kwa kesi ya Freeman Mbowe na wenzake watatu na LHRC dhidi ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 2019 kupinga iliopinga mabadiliko ya Sheria ya Vyama vya Siasa," anasema na kufafanua kuwa ipo sheria inayokataza vyama vya siasa kuungana wakati wa uchaguzi vinginevyo kimoja kife.

Pia, iwapo wapinzani watataka ushirikiano kwenye uchaguzi mgombea wanayemtaka kumsimamisha ndiye anayelazimika kuhama chama lakini si kuunda muungano.

Mwenyekiti huyo wa muda wa kamati ya kukusanya maazimio ya wadau hao anaasema lengo ni kutaka vyama vya siasa kuungana bila vikwazo na kuunda jumuiya kwa maslahi ya taifa ili mabadiliko na uimarishaji wa demokrasia yafikiwe.

Aidha, anasema wanataja kesi nyingine kuwa ni ya Bob Wangwe dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali ya mwaka 2023 iliyopinga wakurugenzi wa halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi.

"Nyingine ni ya Joram Bashange dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa serikali iliyopinga mamlaka ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuwatangaza baadhi ya wagombea kupita bila kupingwa," anakumbusha.

Katika azimio la tisa, anasema wadau wanataka Msajili wa Vyama vya Siasa aitishe mikutano kati ya vyama vya siasa na watu wenye ulemavu ili kuchochea demokrasia shirikishi na ushiriki wao katika michakato ya demokrasia.

"Wadau hao wa demokrasia wameazimia kuhamasisha ushiriki wa vijana katika michakato ya kidemokrasia, ili kuendana na kaulimbiu ya maadhimisho ya Siku ya Demokrasia kwa mwaka 2023 inayosistiza kuwezesha vijana kwa mustakabali wa kizazi kijacho," anasema.

Anataja azimio la 11 kuwa ni lile mashiriki ya kiraia AZAKI kupewa kipaumbele katika kutoa elimu ya mpigakura na kuwa waangalizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka ujao na uchaguzi mkuu wa 2025 ili kuangalia

INAENDELEA UK. 14

MIAKA 24 KUMKUMBUKA MWALIMU

# BBT ilivyowekeza kimkakati kumwenzi Baba wa Taifa



**Na Reubeni Lumbagala, DODOMA**

IMETIMIA miaka 24 tangu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alipotwaliwa katika dunia hii. Pamoja na kwamba, ni miongo miwili sasa imeshaondoka kazi alizoanzisha za kujenga Tanzania bora, zinaendelea na hakuna kurudi nyuma.

Moja ya 'aluta continua' ni kuendeleza kisasa mikakati ya Baba wa Taifa ya kuchochea maendeleo ya kiuchumi yanayogusa maisha ya watu vijijini hadi mijini ikilenga kuboresha na kukuza sekta ya kilimo ambayo ndiyo muhimili wa maisha, inayozihusu karibu sekta nyingine zote.

Kwa Nyerere kilimo ni uti wa mgongo wa taifa, kwani ndiko kinapotoka chakula, ambayo ni mazao mbalimbali mimea na mifugo. Ndiko zinapopatikana malighafi viwandani na ajira ya Watanzania mamilioni.

Nyerere aliamini kuwa Tanzania ni taifa la wakulima na wafanyakazi ambao ni watu muhimu katika kuchochea maendeleo ya nchi yao na vilevile wakati wote alisisitiza kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Tanzania ni kilimo, hivyo ni lazima serikali iweke mazingira mazuri na wezeshi ya kukuza sekta ya kilimo ili kufikia maendeleo ya kweli ambayo kila mmoja aliyatamani.

Katika ukanda wa Kusini ya Jangwa Sahara, Tanzania ni miongoni mwa mataifa machache yenye ardhi kubwa na yenye rutuba kwa ajili ya kustawisha mazao mengi ya chakula na biashara, mathalani, huzalisha mahindi, mpunga, mtama, chai, pamba, katani, kahawa, alizeti, ufuta, ndizi, maharagwe,mbaazi, korosho, mboga za aina zote na matunda.

Kwa mujibu wa Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO), Tanzania ina kilomita za mraba 355,000 za ardhi ya kilimo, sawa na asilimia 40 ya ardhi yake yote, lakini pia inaweza kujitegemea kwa chakula kutokana na kilimo cha umwagiliaji.

Katika maisha yake Mwalimu Nyerere aliamini vijana wenye nguvu ni mtaji muhimu na watawezesha mafanikio ya sekta ya kilimo akiwawekea mkazo na msisitizo mkubwa wa kushiriki kwenye kilimo.

Licha ya kwamba kumekuwa na kusuasua kwa ushiriki wa vijana katika sekta ya kilimo kutokana na wengi wao kupenda kuajiriwa na hasa kupendelea kufanya kazi za ofisini, hali hiyo imewaathiri na sekta ya kilimo pia kwa vile vijana hawakushiriki ipasavyo kwenye kuzalisha mazao mashambani na hata kwenye mifugo na uvuvi.

Vilevile, kumekuwa na mtizamo hasi kwa baadhi ya vijana, wakiamini kilimo si shughuli inayoweza kuwaletea maendeleo ya kiuchumi, na hivyo kukiona kama ni kazi ya watu duni au wazee ambao hawajasoma.

Katika kuboresha sekta ya kilimo na kuongeza ushiriki wa vijana kwenye eneo hilo kama ilivyokuwa malengo ya Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere, Wizara ya Kilimo inatekeleza Programu mahususi ya "Jenga Kesho Iliyo Bora", "Building a Better Tomorrow (BBT)". Ni mradi uliozinduliwa Agosti 2022 na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, katika maonesho ya Sikukuu ya Wakulima au Nanenane kwenye viwanja ya John Mwakangale jijini Mbeya.

Katika uzinduzi huo, Waziri Mkuu Majaliwa anasema: "Vijana wetu fursa ni nyingi nchini kwetu, sekta ya kilimo inazibeba zaidi ya asilimia 50, hatua ya wizara hii kuzindua mpango mkakati wa vijana kuingia kwenye sekta ya kilimo ni mpango unaolenga kuboresha uchumi wa mtu mmoja mmoja kuanzia umri wa vijana."

Akiwahimiza kuwa ni wakati muafaka kwa vijana kuendelea kushiriki programu hiyo ili kukuza sekta ya kilimo, ufugaji na uvuvi na hatimaye kuongeza kipato cha mwananchi na taifa kwa kuwa huko ndiko kwenye sasa au leo na kesho iliyo bora.

Aidha, programu hiyo imelenga kuwaunganisha vijana kutoka maeneo mbalimbali nchini na kuwapa mafunzo bora ya kilimo ili kukuza sekta hiyo kwa ustawi wa vijana na maendeleo ya nchi . Ni mradi ambao pia unakusudia kuwapatia vijana pembejeo bora za kilimo na kuweka mifumo bora na y a kisasa ya umwagiliaji ili kukuza sekta ya kilimo, na hatimaye kupitia uwekezaji huo, Watanzania mijini na vijijini wanufaike na ajira zaidi ya milioni tatu ifikapo mwaka 2030.

Azma ya Mwalimu Nyerere kwenye sekta hiyo ilikuwa ni kukuza kilimo na kuleta mabadiliko ya kilimo nchini kutoka kuwa duni na cha kujikimu hadi cha kisasa na cha kibiashara.

Halikadhalika, programu ya BBT inalenga kutimiza azma hiyo ya Baba wa Taifa kwani BBT inatilia mkazo mageuzi makubwa katika sekta hiyo ili kuchochea ukuaji wa uzalishaji kisasa kwa kutumia teknolojia,pembejeo, mifumo na zana madhubuti zinazoachana na kilimo cha jembe la mkono na kuingia kwenye usasa zaidi.

Vijana hao wanaotarajiwa kulima kupitia mashamba ya pamoja 'block farms' yanawalenga wanufaika wa programu ambao wanapata mafunzo kwa kipindi cha miezi minne katika vituo 15 nchini.

Ili kuondoa vikwazo kwa vijana kushiriki mafunzo haya, serikali inagharamia chakula malazi na mafunzo huku wanufaika wakijigharamia usafiri na mahitaji binafsi pekee wawapo mafunzoni.

Ni jambo la faraja kuona Rais Samia Suluhu Hassan, ansunga mkono juhudi za mwasisi wa taifa hili katika sekta ya kilimo kwa kuhakikisha vijana tena wasomi wanashiriki kikamilifu shughuli za kilimo kwa maendeleo endelevu.

Katika Mkutano wa Jukwaa la Mifumo ya Chakula Afrika (AGRF) unaofanyika Septemba jijini Dar es Salaam, Rais Samia anasema "Lengo la kimkakati la BBT ni kuhamasisha vijana kushiriki katika miradi endelevu kupitia uzalishaji wa mazao, ufugaji na uvuvi, kuwawezesha kupitia mafunzo na ushauri, kuwashirikisha katika usimamizi wenye faida wa kilimo biashara na kuziwezesha biashara zinazoongozwa na vijana kwa kuboresha mazingira ya biashara."

Itoshe kusema, Programu ya BBT chini ya uongozi mahiri wa Rais Samia ni moja ya mradi wenye kumuenzi Mwalimu Nyerere kwa kuhakikisha vijana wanashiriki katika sekta ya kilimo ili kuikuza na kuongeza kasi ya kukuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

**Mwandishi ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali Dodoma.**
**Maoni: 0620 800 462.**

# Uchaguzi mdogo ubunge, udiwani ulivyo muhimu kufikia maendeleo

**Na Bartholomew Wandi**

UCHAGUZI uwe mkubwa au mdogo ni muhimu kukuza demokrasia na kutoa fursa kwa wananchi kuchagua kiongozi wanayemtaka.

Tofauti ya uchaguzi mkuu na uchaguzi mdogo ni kwamba mkuu unahusisha kumchagua rais na wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na madiwani kwa upande wa Bara, Rais wa Zanzibar, wawakilishi, madiwani kwa Zanzibar, ukifanyika kila baada ya miaka mitano.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) huuratibu na kuusimamia, uchaguzi wa Rais na wabunge na madiwani kwa Bara wakati Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) huratibu na kusimamia uchaguzi wa Rais wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na madiwani.

Kwenye uchaguzi huo wapigakura wa Bara hupiga kura tatu kwa wakati mmoja za Rais wa Jamhuri ya Muungano na Makamu mbunge atakayewawakilisha bungeni na diwani ila kwa Zanzibar hupiga kura tano za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wake, Rais wa Zanzibar, mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, mjumbe wa Baraza la Wawakilishi na diwani.

Chaguzi ndogo zipo kwa ajili ya wabunge wa Jamhuri ya Muungano na madiwani wa Bara ambapo kwa Zanzibar huhusisha Rais, wawakilishi na madiwani. Hakuna uchaguzi mdogo wa rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Ibara ya 37 (5) ya Katiba ya Jamhuri ya Tanzania inaeleza kuwa hakuna uchaguzi mdogo wa rais wa Jamhuri ya Muungano na kufafanua kuwa endapo nafasi itakuwa wazi kutokana na rais kufariki dunia, kujiuzulu, kupoteza sifa za uchaguzi au kutomudu kazi zake kutokana na maradhi au kushindwa kutekeleza kazi na shughuli zake, Makamu wa Rais ataapishwa na atakuwa rais kwa muda uliobakia katika kipindi cha miaka mitano.

Aidha, ibara ya 76 (3) ya katiba hiyo ya 1977, kifungu cha 76 (3) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi, sura ya 343 na kifungu cha 13 (6) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa sura ya 292, uchaguzi mdogo wa ubunge na udiwani unafanyika baada ya uchaguzi mkuu wa rais, wabunge na madiwani kupita na haziendelei kufanyika baada ya kubakia miezi 12 (mwaka mmoja) kabla bunge halijavunjwa kupisha uchaguzi mkuu mwingine.

Kwa mantiki hii, NEC hufanya uchaguzi mdogo za ubunge wa Bunge la Jamhuri la Muungano wa Tanzania na diwani Bara. Wakati kwa upande wa Zanzibar, ZEC hufanya uchaguzi wa Rais wa Zanzibar, wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na madiwani. Kwa ufafanuzi huo, Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilifanya uchaguzi wake mkuu wa sita Oktoba 28, 2020 tangu kuanzishwa Januari 13, 1993 baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa mwaka 1992 ambapo, wapigakura15, 094,950, kati ya 29,754,699 walioandikishwa nchi nzima walipiga kura.

Uchaguzi mwingine mkuu wa saba kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977 na sheria za uchaguzi utafanyika mwaka 2025 yaani miaka mitano baada ya ule wa mwaka 2020. Lakini, kipindi cha miaka hiyo mitano kina shughuli nyingi zikiwamo za uchaguzi mdogo ambao hufanyika mara kwa mara kadri sababu zinavyojitokeza.

Tangu uchaguzi mkuu wa Oktoba, 2020 ufanyike mpaka Septemba, 2023, NEC imeshasimamia chaguzi ndogo kadhaa za ubunge na udiwani. Chaguzi hizo ni pamoja na na ule wa ubunge wa majimbo mawili ya Muhambwe na Buhigwe na kata 16 uliofanyika Mei 2021, uchaguzi mdogo wa ubunge Konde, wilayani Micheweni, mkoani Kaskazini Pemba na udiwani kata sita za Bara uliofanyika Julai 18, 2021.




Wapigakura wakitimiza wajibu wa kuwachagua viongozi. **PICHA: MTANDAO**

Ifahamike kuwa chaguzi ndogo nyingine za ubunge na udiwani zilihusisha majimbo ya Ushetu lililoko Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu Shinyanga pamoja na kata tatu uliofanyika Oktoba 9, 2021, na uchaguzi mdogo wa ubunge jimbo la Ngorongoro na udiwani wa kata tano za Tanzania Bara uliofanyika Desemba 11, 2021.

Chaguzi nyingine ni za jimbo la Amani mkoa wa Mjini Magharibi Zanzibar pamoja na wa udiwani wa kata 12 za Bara uliofanyika Desemba 17, 2022, wa madiwani wa kata 14 za Bara wa Julai 13, 2023 na ule wa jimbo la Mbarali, mkoani Mbeya pamoja na kata sita za Barakuchagua madiwani uliofanyika Septemba 19, 2023.

Nini umuhimu wa kufanyika uchaguzi mdogo wa wabunge na madiwani? Tume huitisha uchaguzi mdogo wa ubunge na madiwani kwa sababu ni takwa la kisheria ili mwananchi apate mwakilishi wake baada ya kutokea nafasi wazi kwenye sehemu hizo.

Majukumu ya wabunge wanapochaguliwa ni kuwawakilisha wananchi katika shughuli mbalimbali za maendeleo kuwaongoza kwa makini na uadilifu, kumuuliza Waziri swali lolote kuhusu mambo ya umma hasa kutoka jimboni kwake, kujadili utekelezaji wa kazi kila wizara wakati wa mikutano ya bunge.

Kujadili na kuridhia mpango wowote wa muda mrefu au mfupi unaokusudiwa kutekelezwa na kuutungia sheria ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo, kutunga sheria pale utekelezaji unapohitaji kuwapo na kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa.

Wajibu wa madiwani kwa wananchi wanapochaguliwa ni kuwawakilisha katika shughuli mbalimbali za maendeleo kuwaongoza kwa makini na uadilifu, kusimamia rasilimali na sheria, kugawa rasilimali kwa kufuata taratibu zilizowekwa, kusimamia mchakato wa kutunga na kupitishasheria ndogo katika halmashauri zao, kuiwezesha jamii katika eneo lake kupata fursa mbalimbali za kimaendeleo, kuongoza na kufanikisha kutatua migogoro mbalimbali katika kata, na kuhamasisha shughuli za maendeleo .

Majukumu hayo ya wabunge na madiwani yanaonyesha umuhimu mkubwa wa uchaguzi mdogo wa wabunge na madiwani kwani viongozi kwenye ngazi hizi wanahitajika ili wananchi wapate wawakilishi watakaotatua matatizo yao kupitia vikao vya bunge na vya baraza la wawakilishi.

**Mwandishi ni Ofisa Habari Mkuu Tume ya Taifa ya Uchaguzi.**
**Mawasiliano: 0754203015**

## VITA ISRAEL VS PALESTINA

# Benjamin Netanyahu akosolewa kupambana ili kujitetea kisiasa

**Na Christina Mwakangale**

WAKATI Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, akisema inachokifanya nchi yake dhidi ya Palestina ni kutetea raia wake na kukomesha matukio kama hayo, wachambuzi wa kisiasa wanatazama namna anavyopigana vita, wakisema lengo ni kuokoa nafasi yake kisiasa na urithi wake.

'King Bibi' ndivyo anavyoitwa, anahesabiwa kuwa waziri mkuu wa Israel aliyekaa muda mrefu zaidi katika historia ya nchi hiyo na ambaye amekuwa akijigamba kuwa ameiletea Israel usalama na ustawi zaidi akiwa na miaka 74, anaongoza taifa hilo kwa muda mrefu baada ya kuingia madarakani mwaka 1996 hadi 1999 na baadaye, 2009 hadi 2021 hadi sasa, kwa mujibu wa mtandao wa redio ya RFI.

Wanaodai anapigana na Hamas ili kuokoa nafsi, wanarejea mashtaka ya ufisadi dhidi ya Netanyahu na mkewe Sara wakihusishwa na tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za umma.

Aidha, anajikuta katika hali mbaya sana, huku wengi wakielekeza ukosoaji mkali kwa serikali yake, kwa kile walichokiona kufeli kwa usalama na ujasusi baada ya mashambulizi ya Hamas. Mashambulizi kati ya Israel kwenda Gaza, yameingia siku ya 10 kwa kuzingatia mwendelezo wa mashambulizi ya anga, baharini na ardhini yanayotekelezwa na Israel huko Ukanda wa Gaza.

Ni baada ya Hamas na makundi ya Palestina kulipua miji ya Israel kwa makombora, kufanya operesheni za kujipenyeza katika maeneo yanayozunguka Gaza na kukabiliana na wanajeshi wa Israel. Kuna mpangilio wa matukio muhimu zaidi yaliyotokea wakati wa siku 10 za mashambulizi hayo, taarifa rasmi ya kwanza kutoka kwa Hamas ilitolewa na kamanda wa Brigedi za Izz al-Din al-Qassam, tawi la kijeshi la harakati ya Hamas, Muhammad al-Deif, akitangaza katika ujumbe uliorekodiwa uzinduzi wa Operesheni "Mafuriko ya Al-Aqsa."

Anasema ulikuwa wakati wa adui kuelewa kwamba muda wa sherehe bila kulipa umeisha. Akiwataka Wapalestina kushambulia makazi ya Israel kwa silaha zote walizonazo.



Na zaidi ya saa moja, baada ya kuanza kwa operesheni hiyo, jeshi la Israel lilitangaza wanamgambo wa Hamas wameingia katika maeneo ya kusini mwa nchi hiyo na kuwataka wakazi wa mji wa Sderot na mingine kubakia nyumbani kwao.

Katika vita ya sasa takribani watu 3,000 wamepoteza maisha katika eneo la Gaza, baada ya kundi la wapiganaji wa Hamas ambalo ni mojawapo ya makundi kadhaa ya wapiganaji wa Kipalestina ambayo yanadhibiti ukanda wa Gaza, kuishambulia Isarel takriban wiki mbili sasa.

Israel ilitangaza vita na kutoa wito wa askari wa akiba, ili kukabiliana na mashambulizi ya roketi kutoka Gaza, pia ikianza kwa operesheni za kukabiliana na Hamas. Ndege za kwanza za kivita zilishambulia Ukanda wa Gaza. Saa moja baadaye, Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, akitoa kauli yake ya kwanza kuhusu kile kilichokuwa kikitokea mtandaoni akisema, Israel iko katika vita.

Kufikia saa 6:00 mchana, baada ya shambulizi, jeshi la Israel lilianza kufanya operesheni za kupambana na Hamas kusini mwa ncho hiyo, huku makombora yakirushwa kutoka Gaza katika maeneo hayo yakiongezeka kila wakati na kufikia zaidi ya roketi 1,200.

Hamas ilitoa kanda za video zinazoonyesha operesheni zake dhidi ya maeneo ya jeshi la Israel na mafanikio yake kwa kuwakamata wanajeshi wake, video pia zikionyesha utekaji nyara wa raia wa Israel wanaoishi katika miji inayozunguka Gaza na uhamisho wao hadi Ukanda wa Gaza.

Sambamba na hayo, Marekani ikatoa tamko la kwanza kupitia Baraza la Usalama la Taifa, likilaani kile ilichokitaja kuwa ni shambulio la kigaidi na kuthibitisha uungaji mkono wa Marekani kwa Israel. Rais Marekani Joe Biden, akimpigia simu Netanyahu kueleza rambirambi zake na kumuunga mkono na baadaye akatangaza katika hotuba yake kwamba uungaji mkono utakwenda sambamba na wa kijeshi.

Kwa mujibu wa BBC vita vinavyoendelea kati ya vuguvugu la Hamas na makundi mengine ya Wapalestina yenye silaha katika Ukanda wa Gaza dhidi ya Israel ni sehemu mpya katika mfululizo unaoendelea wa vitendo vya ukatili, mauaji na mashambulizi ya kujitoa mhanga tangu kuanzishwa kwa vuguvugu la Hamas mwaka 1987 na mwasisi wake Mpalestina Ahmed Yassin.

Pamoja na Hamas, kundi la Hezbollah lipo kwenye mzozo huo lilifanya shambulio la kombora kwenye eneo la jeshi la Israeli kwenye mpaka na Lebanon, lililoua ofisa wa jeshi la Israeli. Hezbollah ilitangaza tangu mwanzo wa vita kwamba linaunga mkono mashambulizi ya Hamas, lakini ilijibiwa kwa kushambulia kwa mabomu maeneo ya karibu ya miji ya Lebanon kwenye mpaka na Israel.

Waziri wa Ulinzi wa Israel alitangaza amri ya kukata umeme, maji na kuzuia kuingia kwa chakula na mafuta katika Ukanda wa Gaza. "Tunapambana na binadamu wanyama," anasema. Israel ilituma ndege za usafiri za C-130 hadi Ulaya kuwasafirisha wanajeshi waliokuwa likizo na kuwarejesha nchini kushiriki katika vita hiyo, BBC inasema.

## WATETEZI DEMOKRASIA WATAKA UWAZI KATIBA MPYA, MGOMBEA HURU, VYAMA KUUNGANA

**INATOKA UK. 11**

ufuatwaji na utekelezaji wa haki za binadamu na demokrasia ya vyama vingi.

"Vilevile wanatamani viongozi wa kitaifa waonyeshe kwa vitendo kauli chanya wanazizotoa hadharani, ili kurudisha na kuimarisha imani ya wananchi kwa serikali yao na katika azimio jingine wanaitaka serikali ikubali ripoti ya tathmini kuhusu mchakato wa katiba mpya iliyotolewa na kikosi cha wataalamu wa Umoja wa Mataifa ya mwaka 2022 ya UN Technical and Financial Support Group)," anasema Kibanda.

Kibanda pia anasema kuwa wanaazimia kuongeza jitihada za makusudi, ili ushiriki wa wanawake katika mchakato wa uchaguzi bila wanaume kuogopa kuwa nafasi zao za sasa zitachukuliwa na wanawake.

Ataja azimio jingine la wadau hao kuwa ni kutaka mchakato wa kutungwa sheria uwe wa wazi na shirikishi ili umma ushiriki katika mchakato huo kwa kutoa maoni badala ya kupitishwa kwa haraka chini ya hati ya dharura.

"Hata hivyo, wanawagusa wananchi kwa kuwataka waache mtindo wa kulalamika bila kutoa mapendekezo ya maboresho katika maeneo yenye changamoto na kuwe na utaratibu wa kufikisha mapendekezo hayo kwenye ngazi zinazokusudiwa," anasema.



# Wenye mabucha waonywa tabia kubeba nyama begani

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAHUDUMU wa bucha za nyama jijini Dodoma wametakiwa kuacha tabia ya kubeba nyama mabegani, badala yake watumie vyombo maalumu vinavyostahili ili kulinda afya za walaji.

Mkurugenzi wa Kampuni ya Talibo Traders Company LTD inayojihusisha na uuzaji wa nyama pori jijini hapa, Nelson Talibo alisema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu usalama wa nyama katika bucha.

Aidha, aliwataka wahudumu hao wa mabucha kupima afya zao mara kwa mara ili kujilinda na maambukizi ya magonjwa yanayoweza kuwapata wao pamoja na watumiaji wa nyama hizo.

Mkurugenzi huyo aliwataka pia wahudumu hao kutumia vyombo vya kisasa vya kubebea nyama badala ya kutumia mabega na kujitwisha vichwani kwa kuwa hali hiyo inaweza kusababisha kwa asilimia kubwa kuwepo kwa maambukizi ya magonjwa kwa pande zote mbili.

"Wahudumu walio wengi nyama zinapoletwa kwenye mabucha baadhi yao badala ya kubebea kwenye vyombo vya kisasa vinavyostahili wanatumia mabega na vichwa vyao kubebea nyama hizo hali ambayo ni hatari kiafya," alisema.

Hata hivyo, aliwataka walaji wa nyama kujihadhari na matumizi ya nyama zinazouzwa mitaani kwa kuwa zilizo nyingi zimekosa vigezo kutokana na kuchinjwa bila kupimwa na wataalamu wa afya.

Hata hivyo, aliwaomba wamiliki wa mabucha kuhakikisha wanajipanga kiafya kwenye maeneo yao, hii ni pamoja na wafanyakazi kuwa na sare na wanapimwa afya kwa lengo la kujilinda na maambukizo ya magonjwa.

# Kongwa yapokea milioni 238/- uboreshaji miundombinu ya maji

**Na Paul Mabeja,** KONGWA

WILAYA ya Kongwa mkoani Dodoma, imepokea Sh. milioni 238 kutoka Programu ya "P4R" inayotekelezwa na Benki ya Dunia (WB) na Serikali ya Tanzania kwa lengo la kuboresha miundomhinu ya majisafi na usafi wa mazingira.

Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Mwema, aliyasema hayo kwenye kikao cha Kamati ya Afya ya Msingi (PHC) wakati akiwasilisha mada kuhusu mradi huo unaolenga uendelevu wa maji na usafi wa mazingira.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha jamii inaishi kwenye mazingira mazuri.

Mwema alisema katika wilaya yake, programu hiyo inatekelezwa katika zahanati tatu za Manyata, Hembahemba na Msunjilile ambazo zimetengewa Sh. bilioni 160.7 na CHMT ikitengewa Sh. milioni 78.1.

Kadhalika, aliwataka wasimamizi wa miradi ya kijamii wilayani humo inayotumia fedha za umma kuandaa bajeti zenye tija, ili kuyafikia malengo ya miradi hiyo badala ya kuweka vipaumbele kwenye malipo ya posho na maslahi binafsi.

Pia alisisitiza mapitio ya bajeti katika mradi wa "P4R" yanapaswa kutiliwa mkazo ikiwa ni pamoja na kuleta matokeo chanya kwenye jamii, suala la tahadhari ya mlipuko wa ugonjwa wa surua likisimamiwa kikamilifu.

Naye Mratibu wa Chanjo na Mnyororo Baridi Kongwa (DIVO), Cosmas Mlimila, alitoa tahadhari ya mlipuko wa ugonjwa wa surua na kusisitiza kuwa chanjo kwa watoto wote ambao hawakukamilisha au kutochanja kabisa inatarajiwa kutolewa kwa misingi ya dharura.

Mlimila alizitaja dalili za ugonjwa wa surua kuwa ni pamoja na homa kali, vipele, macho kuwa mekundu, kikohozi na mafua na athari zake zikiwa ni nimonia kali, upofu wa macho, homa ya uti wa mgongo na hatimaye kifo.

Alisema ugonjwa wa surua husambazwa kwa njia ya kikohozi au chafya kutoka kwa mtu aliyeambukizwa na dalili zake huonekana kuanzia siku saba hadi 18.

Aliitaja mikakati ya kukabiliana na ugonjwa wa surua wilayani hapo, kuwa ni pamoja na kuwatafuta watoto wote ambao hawajakamilisha chanjo au kutochanja kabisa, utoaji wa elimu kwa jamii na kurahisisha upatikanaji wa chanjo ili kuimarisha huduma za mkoba.

Ofisa Afya Wilaya ya Kongwa, Abdulrahman Shehe Othman, alisema malengo ya mradi huo ni pamoja na kuboresha miundombinu ya maji na usafi wa mazingira katika vituo vya kutolea huduma za afya katika halmashauri.

Pia kuhamasisha ujenzi na matumizi ya vyoo bora katika ngazi ya kaya pamoja na kuhimiza tabia ya kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni.



Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza, (SACP) Athuman Kitiku, akizungumza wakati wa kufungua mafunzo kwa wastaafu watarajiwa wa Jeshi la Magereza yaliyofanyika jijini Dodoma jana, yaliyoandaliwa na Benki ya NMB kupitia Kampeni ya Huduma kwa Wastaafu ijulikanayo Hekima Plan. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Rais Samia akerwa vituo 15 vya afya kutofanya kazi

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

RAIS Samia Suluhu Hassan amesikitishwa na kitendo cha vituo 15 vya afya ambavyo serikali ilitoa fedha kuvijenga mkoani Singida kuchelewa kuanza kutoa huduma, kwa sababu ambazo hazieleweki.

Aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wananchi kwenye mkutano wa hadhara ukiofanyika mjini Singida kwenye maadhimisho ya kumbukizi ya Mkoa wa Singida kutimiza miaka 60 tangu ulipoanzishwa Oktoba 15, 1963.

"Serikali imejitahidi kujenga vituo vya afya nchi nzima lakini kwa sababu zisizoeleweka zaidi ya vituo 15 vimechelewa sana kufunguliwa vifaa tiba vipo na labda watumishi wamekuwa wakiletwa lakini huduma hazijaanza," alisema.

Rais Samia alisema katika suala hilo ni tabia za watu tu na hivyo kuagiza viongozi wa Mkoa wa Singida kubadilika pamoja na changamoto zilizopo, lakini nguvu zaidi zielekezwe kwenye matumizi ya fursa zilizopo.

Alisema viongozi wa Singida wanapaswa kubadilika kwa kutumia fursa zilizopo kuleta maendeleo kwa wananchi na kutoa mfano Mkoa wa Singida kuna hekta 26,823 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji.

"Lakujiuliza Singida ni ile ile toka ilivyoumbwa kama ni mvua inanyesha, lakini pamoja na suala la mabadiliko ya tabia ya nchi sasa tuelekee kwenye mabadiliko ya watu na kutoka hapo ndiyo tuongeze uzalishaji," alisema.

Aidha, Rais Samia aliwataka wananchi kuchukua tahadhari kutokana na uwezekano wa kunyesha mvua za El - Nino ambazo zinaweza kuleta athari hususani kwa wananchi wanaoishi mabondeni.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, alisema katika kipindi cha miaka miwili sekta ya afya imeimarika kwa kusogeza huduma kwa wananchi, miundombinu ya afya iliyojengwa na kukamilishwa imesaidia wananchi kuwa na uhakika wa kupata matibabu.

Alisema katika kipindi hicho mkoa ulipokea Sh.bilioni 51.5 ambazo zimetumika katika ujenzi wa hospitali nne mpya, ukarabati wa hospitali moja, ujenzi wa vituo vya afya 22 na ukamilishaji wa zahanati 69.

Alisema fedha hizo pia zimetumika kujenga majengo matatu ya dharura, majengo mawili ya wagonjwa mahututi na ujenzi wa nyumba sita za makazi ya watumishi wa afya, ununuzi wa vifaa tiba na dawa kwenye hospitali za wilaya saba, vituo vya afya 22 na zahanati 220.





# Daladala zagoma, washinikiza serikali kupandisha nauli

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHUGHULI za kiuchumi ikiwamo usafiri na usafirishaji zimesimama kwa zaidi ya saa 10 mkoani Mbeya baada ya wamiliki wa magari ya kusafirisha abiria kugoma, ili kushinikiza serikali kupandisha nauli kutokana na ongezeko la bei ya mafuta.

Mgomo huo ulianza juzi majira ya saa 12 asubuhi ukihusisha magari yote ya abiria yanayofanya safari zake katikati ya Jiji la Mbeya maarufu kama daladala na yale yanayoanzia safari zake ndani ya jiji hilo kwenda wilayani na mikoa jirani.

Wakieleza sababu za mgomo huo, baadhi ya madereva wa magari hayo walisema kuwa wamelazimika kusitisha huduma na kuondoa magari yao barabarani kutokana na mafuta kupanda bei, huku nauli za kusafirisha abiria zikibakia zile zile.

Mmoja wa madereva hao, Elia Chimpinda alisema nauli wanazotoza abiria wao haziendani na bei ya mafuta, hali ambayo inasababisha wapate hasara na kushindwa kuendesha biashara hiyo.

"Kwa sasa mafuta yamepanda bei kwa kiwango kikubwa ambacho ukilinganisha na viwango vya nauli tunavyowatoza abiria wetu tunapata hasara, hivyo hatuwezi kuvumilia ndio sababu tumesitisha huduma ili serikali iridhie kuongeza nauli," alisema Chimpinda.

Kwa upande wake Shakir Gadi ambaye ni dereva wa gari la abiria, alisema kuwa viwango vya nauli vinavyotumika kwa sasa vimepitwa na wakati kutokana na maisha kupanda, huku bei ya mafuta ikiwa juu.

"Ukipandisha bei ya mafuta ujue maisha kwa ujumla yanapanda ikiwamo bei ya vipuli vya magari, lakini serikali haitaki tupandishe nauli jambo ambalo sisi tunaona sio sahihi na ndio maana tumelazimika kusitisha huduma zetu," alisema Gadi.

Nao baadhi ya abiria waliokuwa wamekwama kwenye maeneo mbalimbali wakisubiri usafiri walisema mgomo huo unaathiri uchumi wao kutokana na nauli kuongezeka mara dufu.

Mmoja wa wananchi hao, Aziza John alisema kutokana na mgomo huo walikuwa wanalazimika kusafiri kwa kutumia bajaji ambazo badala ya kulipa nauli ya Sh. 500 walioyozoea walianza kulipa Sh. 2,000.

Kufuatia mgomo huo, Uongozi wa Wilaya ya Mbeya ulilazimika kuita kikao cha dharura na wamiliki wa magari hayo pamoja na Maofisa wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kutafuta suluhu ya mgomo huo.

Kikao hicho cha dharura kilifanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya na baada ya kumalizika, Ofisa Mfawidhi wa LATRA Nyanda za Juu Kusini, Omary Ayoub, alisema wamekubaliana wamiliki kusitisha mgomo huo na kuendelea kutoa huduma.

Alisema pia wamekubaliana kuendelea kutumia viwango vile vile vya nauli vilivyowekwa na serikali mpaka hapo serikali itakapokutana na wamiliki wa vyombo vya usafiri kupanga viwango vipya vya nauli.

Alisema serikali kupitia LATRA makao makuu imepanga kukutana na wamiliki wa vyombo vya moto Oktoba 18, mwaka huu jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kupitia viwango vya nauli.

Kutokana na makubaliano hayo Ayoub alisisitiza kuwa viwango vya nauli vitaendelea kutumika vile vile vya zamani na kwamba mtoa huduma yeyote atakayepandisha nauli kabla ya serikali kutangaza viwango vipya atachukuliwa hatua.

Kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta, madereva na makondakta wa magari ya abiria walipandisha nauli kinyemela ambapo katika maeneo ambayo abiria walikuwa wanalipa Sh. 550 walipandisha mpaka Sh. 700, huku maeneo ambayo ilikuwa Sh. 1000 ikifikia 1,400.




Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Ndege ya 'Air France KLM kwa nchi za Afrika Mashariki, Nigeria na Ghana, Marius van der Ham (kushoto), akikata keki na Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Nabil Hajlaoui, wakati wa kusherehekea miaka 90 ya kampuni hiyo jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# DC atangaza kiama kwa wanaochoma moto misitu

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, imewatangazia kiama watu wanaoharibu mazingira wilayani hapa kwa kuchoma moto kwenye misitu, hali ambayo inasababisha mabadiliko ya tabianchi na kusababisha baadhi ya wanyama kuhama.

Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Jafaru Haniu alitangaza kiama hicho juzi alipofanya ziara ya kukagua uharibifu wa mazingira kwenye Hifadhi ya Mazingira Asilia ya Mlima Rungwe hasa kwenye Msitu wa Uporoto lilipo Ziwa Ngosi na kubaini baadhi ya maeneo yakiwa yamechomwa moto.

Haniu aliagiza ulinzi na usalama wilayani hapa kushirikiana na maofisa wa Wakala wa Huduma za Misitu nchini (TFS) kuwasaka na kuwachukulia hatua za kisheria watu wote wanaochoma moto kwenye maeneo hayo.

Alisema amebaini kuwa baadhi ya watu wanachoma misitu hiyo nyakati za usiku ili wasibainike jambo ambalo linasababisha kuwabaini kuwa vigumu na hivyo akavitaka vyombo vya ulinzi kutumia mbinu za kiintelijensia kuwabaini.

Alisema msitu huo umehifadhiwa kiasili ili kulinda Ziwa Ngosi, vyanzo vya maji, miti ya asili pamoja na viumbe wengine wadogo wakiwamo wanyama ambao ndio vivutio vya watalii.

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Safu za Mlima Rungwe, Grace Wille, alisema misitu hiyo ni moja kati ya vivutio vya watalii vilivyomo katika wilaya hiyo na kwamba inapochomwa uzuri wake unapotea.

Alisema wapo baadhi ya wanyama ambao wanaishi kwenye misitu hiyo lakini huwa wanahama kutokana na misitu kuchomwa moto hali ambayo inasababisha ugumu wa watalii kufikia.

Hivyo, aliwaomba wananchi wanaoishi jirani na safu za mlima huo kushiriki kwenye utunzaji wa mazingira ili na wao waendelee kufaidi matunda ya viumbe hai waliomo pamoja na maliasili zingine.

## Ujenzi wa barabara njia nne Mbeya waanza kwa 'speed'

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UJENZI wa barabara ya njia nne (km. 29) kutoka Nsalaga jijini Mbeya mpaka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA), umeanza kushika kasi, ambapo nyumba zote zilizopo kwenye maeneo ya hifadhi ya barabara hiyo zimeanza kubomolewa.

Ujenzi wa barabara hiyo ulikuwa umesimama kutokana na miundombinu mbalimbali ikiwamo ya maji, umeme, mawasiliano na baadhi ya nyumba kuchelewa kuondolewa.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wakazi wa mkoa huo wameiomba serikali kumsimamia mkandarasi anayejenga barabara hiyo kuendelea na kasi aliyoanza nayo sasa ili mradi ukamilike haraka na kuondoa kero zilizopo hasa msongamano wa magari katikati ya Jiji.

Mmoja wa wananchi hao, Stefano Mwasile alisema miundombinu ambayo ilikuwa inaonekana kuwa kikwazo kwenye barabara hiyo imeshaondolewa na hivyo kazi iliyobaki ni kwa mkandarasi kuongeza kasi.

Alisema katika baadhi ya maeneo wamekuwa wakikumbwa na mafuriko kutokana na kutokana na mitaro kuwa midogo na kwamba barabara hiyo ikikamilika huenda wakaondokana na adha hiyo.

"Huu mradi tumeusubiri kwa muda mrefu sana, wenzetu Iringa na Njombe ulishakamilika na barabara ni zuri sana, tatizo ni kuanzia Igawa mpaka Tunduma, kwa hili eneo ambalo wameamua kuanzia ni muhimu sana," alisema Mwasile.

Naye Raphael Mboya alisema wapo baadhi ya wananchi ambao walishalipwa fidia muda mrefu lakini walikuwa hawataki kuhama jambo ambalo liligeuka kuwa kero.

Alisema kwa sasa baada ya kubomoa nyumba zao wameanza kuona kasi ikiongezeka na kwamba mradi huo ukikamilika utasaidia kupunguza ajali za barabarani ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara.

Hivi karibuni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alimtaka mkandarasi ambaye ni Kampuni ya CHICO ya nchini China kuanza ujenzi kwa kuanzia katika eneo la Ifisi ambako kulikuwa hakuna miundombinu mingine.





## Jamii yatakiwa kutoa kipaumbele matatizo ya afya ya akili

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

DAKTARI Bingwa wa Magonjwa ya Afya ya Akili kutoka Hospitali ya Wagonjwa wa Akili Kidongochekundu Zanzibar, Khadija Abdulrahman, ameitaka jamii kutoa kipaumbele kwa matatizo ya fya ya akili badala ya kujikita zaidi kwenye afya ya mwili.

Aliyasema hayo visiwani hapa wakati wa hafla ya uoneshaji wa kazi za nasaa zinazofanywa na wagonjwa wa afya ya akili.

Daktari huyo alisema hali hiyo inachangia wagonjwa kuchelewa kupona au kupata nafuu na hivyo kuongeza ukubwa wa tatizo.

Alisema watu wenye changamoto za afya ya akili wana haki ya kuthaminiwa, kutibiwa na kupata matunzo kama ilivyo kwa wagonjwa wa maradhi mengine na kitendo cha kuwatenga ni ukiukaji wa haki za binadamu.

"Tumeona watu wengi wenye changamoto hii sehemu mbalimbali wakidharauliwa, kunyanyaswa, kuchekwa, kuchokozwa, watoto kubakwa kwa sababu tu ya ugonjwa walionao. Hii si sawa kwani hata Shirika la Afya Duniani (WHO) linahimiza watu hawa watunzwe na kuthaminiwa," alisema.

Alisema lazima kila mmoja kutambua haki za watu hao ambao kimsingi hawakupenda kuumbwa katika hali hizo na changamoto hiyo isiwe sababu ya kutendewa kinyume na haki za binadamu.

Akizungumzia kazi za mikono wanazofanya ikiwemo kuchora picha, kusuka ukili na mikoba, kufuma na kuchonga, Dk. Khadija alisema hiyo ni dalili ya vipaji walivyonavyo ambavyo vinafaa kuendelezwa kama sehemu ya tiba ili kuwaponesha.

Hivyo, alikishukuru Chuo Kikuu cha Auckland nchini Norway kwa msaada wao wa kujenga kituo maalum katika Hospitali ya Kidongochekundu ambacho wagonjwa wanakitumia kutengeneza vitu mbalimbali na kuharakisha kupona kwao.

Aidha, alifarijika na jitihada za Kituo cha Sanaa Zanzibar (CUAGA-Cultural Arts Gallery) pamoja na Wakfu wa Emerson Zanzibar kwa kushirikiana katika kudhamini na kuandaa maonesho ya kazi hizo za mikono kwa lengo la kuielewesha jamii uwezo na haki za watu wenye changamoto hiyo.

Ramadhani Seif Ramadhan, ni miongoni mwa wachoraji kutoka hospitali hiyo, alisema amekuwa na kipaji hicho tangu akiwa na umri wa miaka 10 na katika maonesho hayo amechangia picha nne.

Aliiomba serikali kuangalia uwezekano wa kulitanua eneo wanalofanyia kazi katika Hospitali ya Kidongochekundu na kuliwekea miundombinu ili kuchukua watu wengi zaidi kuendelea kupata tiba kwa kazi za mikono.

Aidha, aliitaka jamii iache tabia ya kuwanyanyapaa watu hao na badala yake washirikiane nao kwa sababu hakuna anayeijua kesho yake.

# Serikali yapokea 'vifaranga' 60,000 vya samaki kutoka Indonesia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar imepokea vifaranga vya samaki 60,000 aina ya mwatiko kutoka Indonesia kupitia Kampuni ya Zanzibar Marine Haerchery hali itakayoondoa uhaba wa bidhaa hiyo nchini.

Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk.Aboud Suleiman Jumbe akizungumza baada ya kupokea na kuhifadhiwa kwa vifaranga hivyo alisema kwa muda mrefu Zanzibar imekua ikikabiliwa na matatizo ya teknolojia na rasilimali, hivyo kwa sasa wananchi watanufaika na vifaranga hivyo.

Alisema kuwa mfumo wa ushirikiano kati ya sekta binafsi na serikali umefanikiwa kuondoa tatizo hilo la kutokuwepo kwa vifaranga vya samaki Zanzibar. Alisema wizara hiyo ina matarajio ya kupokea vifaranga wengine aina hiyo 50,000 ndani ya mwezi huu na kuondoa uhaba wa samaki kwa muda mrefu.

Alisema kuwa vifaranga hivyo vilivyoletwa viko salama wala havijatumia kemikali ya aina yoyote, hivyo wananchi wanatakiwa kuzidi kuandaa mashamba yao kwa ajili ya ufugaji wa samaki. Mmoja wa wakurugenzi wa Kampuni ya Zanzibar Marine Hearchery, Ibrahim Faisal Shah alisema wataendelea kushirikiana na serikali juu ya upatikanaji wa vifaranga zaidi ili kuondoa uhaba wa bidhaa hiyo nchini.

Aidha alisema kuwepo kwa vifaranga hivyo ni moja ya juhudi kubwa za seriakli katika kuhakikisha kuwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inawanufaisha wananchi wa Zanzibar kupitia rasilimali za baharini.



Hassan Nemshi, Mkazi wa Kijiji cha Paje Mkoa wa Kusini Unguja akifuma kuti jana kwa ajili ya kuezeka nyumba yake. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Makamu wa Rais ahimiza utoaji elimu ya majanga katika jamii

**Na Mwandishi wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdullah amewataka viongozi wa taasisi zinazohusika na kukabiliana na maafa kutoa elimu kwa jamii juu ya majanga na jinsi ya kutumia rasilimali zilizopo katika kujikinga, ili kunusuru maisha ya wananchi na mali zao.

Aliyasema hayo katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kukabiliana na Maafa Duniani yaliyofanyika visiwani hapa.

Alisema kuwa lengo kuu la kuadhimisha siku hiyo ni kuihamasisha jamii pamoja na taasisi mbalimbali kutekeleza wajibu wao katika kupunguza uwezekano wa kukumbwa na maafaa pamoja na kukumbushana wajibu wa kuchukua hatua za kujikinga na majanga yanayosababishwa na binadamu.

Pia kupunguza athari kwa majanga ya kimaumbile sambamba na kujiandaa kukabiliana na kurejesha hali baada ya kutokea maafa.

Hemed alisema kuwa kuongezeka kwa matukio ya majanga yakiwemo ya matetemeko ya ardhi, upepo mkali, kuzama kwa meli na ajali za barabarani pamoja na majanga ya moto ambayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara katika visiwa vya Zanzibar yanasababisha kuwepo kwa jamii kubwa tegemezi na yenye uwezo mdogo katika kukabiliana na kurejesha hali wakati na baada ya maafa kutokea.

Hivyo, alitoa wito kwa taasisi zote zenye miradi ya ujenzi kuhakikisha zinashirikina na kamisheni ya kukabiliaba na maafa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kabla, wakati na baada ya ujenzi ili kuhakikisha uwepo wa mipango na miundombinu ya kukabiliana na majanga.

Aidha, aliwataka madereva kufuata sheria za usalama barabarani ili kuepusha ajali zisizo za lazima pamoja na Jeshi la Polisi liendelee kusimamia sheria hizo ikiwemo kuwachukulia hatua wale wote wanaokiuka.

Aidha, alizitaka serikali za mikoa na wilaya kusimamia ujenzi kwa mipango ili kuepusha ujenzi holela katika jamii, hatua ambayo itasaidia kupambana na majanga yatakapotokea.

Naye Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma alivishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa Jitihada zao wanazozichukua panapotokea majanga ili kunusuru wananchi na mali zao.

Aliwataka wananchi kutumia namba za dharura 114 kwa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na 190 kwa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kwa kutoa taarifa zozote za majanga ili kuzirahisishia kamati za kukabiliana na maafa kufika kwa muda kudhibiti maafa yanapotokea.

Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa (UN), Dorothy Temu Usiri alisema UN unatambua na kuthamini juhudi zinazofanywa na Serikali kwa kuhakikisha wanakabiliana na majanga yanapotokea pamoja na juhudi ya kuwa na mpango wa kukabiliana na Mvua za El-Nino zinazotabiriwa kunyesha hivi karibuni.

Alisema utayari wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wadau wa maendeleo unaendelea kuimarika ambapo mashirika ya UN yataendeleza kuunga mkono juhudi hizo ili kukabiliana na majanga ambayo yanachangia kuongezeka kwa umasikini duniani.

Msaidizi Mrakibu wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Makame Omar Moh'd alisema kuwa wameanza kujenga mabomba yatakayosaidia kudhibiti moto kwa wepesi, hatua ambayo itasaidia kurahisisha uzimaji wa moto utakapotokea.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VYETI VIMEPOTEA



**CLOTILDA WILLIAM MAHIMBO** anatangaza kupotelewa na cheti chake cha taaluma cha shahada ya uzamili cha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania pamoja na hati ya matokeo ya mitihani ya shahada ya uzamili, yenye namba ya usajili Pg201608711vilivyotolewa mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeviona au atakayevipata awasiliane kwa namba 0752 – 056031 au atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**RB: PHQ/MWA/MAG/4558/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

HABIU DAUDI SEMLANGWA anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye namba ya usajili MC 874 CVH.kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

PHQ/TAN/MUH/1835/2023

## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI

UMOJA WA DEREVA BAJAJI IRINGA UNATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI TATU ZA BAJAJI MC 205 DFF RANGI YA KIJANI, MC 206 DFF RANGI YA BLUU, MC 207 DFF RANGI NYEKUNDU, YEYOTE ATAEFANIKIWA KUZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

POLISI JALADA NAMBA

PHQ//IRI/2185/2023.

PHQ/IRI/IRI/2184/2023.

PHQ/IRI/IRI/2186/2023.


## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI

UMOJA WA DEREVA BAJAJI IRINGA UNATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI TATU ZA BAJAJI MC 205 DFF RANGI YA KIJANI, MC 206 DFF RANGI YA BLUU, MC 207 DFF RANGI NYEKUNDU, YEYOTE ATAEFANIKIWA KUZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

POLISI JALADA NAMBA

PHQ//IRI/2185/2023.

PHQ/IRI/IRI/2184/2023.

PHQ/IRI/IRI/2186/2023.


## KUPOTEA KWA KADI ZA BAJAJI

UMOJA WA DEREVA BAJAJI IRINGA UNATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI MBILI ZA BAJAJI ZENYE USAJILI MC 203 DFF RANGI NYEUSI, MC 199 DFF RANGI NYEUSI, YEYOTE ATAEFANIKIWA KUZIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE,POLISI JALADA NAMBA

PHQ/IRI/IRI/2183/2023.

PHQ/IRI/IRI/2087/2023

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 30 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE**
**VERONICA LEONARD DAFFA**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY JULIUS RAJABU MBWAMBO**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Admnistration is made to the above named petitioner

Objections to the grant should be filed on or before the 16th day of November 2023

Dated at Korogwe this 16th day of October 2023

RESIDENT MAGISTRATE
KOROGWE

---

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZNAIA**
**JUDICIARY**
**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF ARUSHA**
**AT ARUSHA**
**EXCUTION CASE NO. 24 OF 2023**
**OLASIT INVESTMENT............... DECREE HOLDER**
**VERSUS**
**RASHID SEIF T/A IPTISAM TRANSPORT LTD......JUDGEMENT DEBTOR**
**Notice to show cause why Warrant of Arrest should not issue**
**( O.XX,R.35 (1) of the Civil Procedure Code)**

**TO:**
**RASHID SEIF**
**P.O.BOX 249**
**TANGA.**
**0753 747 494.**

Whereas Decree Holder named above has made application to this Court for execution of decree in this case by arrest and imprisonment of you in person.

You are hereby required to appear before this Court on the 30th day of October.2023 at 8:00 am in the forenoon to show cause why you should not be committed to the CIVIL Prison in execution of the said decree.

GIVEN under my HAND and SEAL of the Court this 11th day of October ,2023

Resident Magistrate
ARUSHA.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

NADIR SAID SALIM anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya HONDA yenye usajili namba MC 965 CRM .Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

PHQ/DAR/TEM/26971/2023

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TARIME**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 40 YA 2020**
**ALBETUS OTIENO SAUSI.... MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1. SARONGE MATOYO**
**2. ANNA SARONGE MATOYO........WAJIBU MAOMBI**

**WITO WA KUITWA SHAURINI**

**KWA: SARONGE MATOYO POPOTE ULIPO**

UNAFAHAMISHWA KWAMBA MLETA MAOMBI HAPO JUU AMELETA MAOMBI MADOGO NAMBA 40/2020 DHIDI YAKO KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYANI TARIME, OMBI LIMEPANGWA KUSIKILIZWA TAREHE 01/11/2023 KWA HIVYO UNATAKIWA KUHUDHURIA KATIKA BARAZA SIKU HIYO WEWE WENYEWE , WAKILI WAKO AU MTU MWINGINE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUJIBU OMBI HILO.

KAA- UKIJUA KUSHINDWA KUFIKA BARAZA LITASIKILIZA OMBI HILO NA KUTOA UAMUZI BILA WEWE KUWEPO.

IMETOLEWA NAMI KWA AMRI NA CHAPA YA BARAZA LEO TAREHE 13/10/2023.

**MAHELELE MUSA SUKUMBA**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) TARIME**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA TARIME**
**MAOMBI MADOGO NAMBA 102 YA 2023**
**PETER CHACHA KITANG'ITA.... MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1.CHARLES MSETI**
**2.EXIM BANK (T) LTD**
**3. GETRUDA CHARLES MSETI........WAJIBU MAOMBI**

**WITO WA KUITWA SHAURINI**

**KWA:CHARLES MSETI NA GETRUDA CHARLES MSETI.**

MNAFAHAMISHWA KWAMBA MLETA MAOMBI HAPO JUU AMELETA MAOMBI MADOGO YA KUKAZIA HUKUMU NAMBA 102/2023 DHIDI YENU KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYANI TARIME, OMBI LIMEPANGWA KUSIKILIZWA TAREHE 25/10/2023 KWA HIVYO MNATAKIWA KUHUDHURIA KATIKA BARAZA SIKU HIYO NYIE WENYEWE , WAKILI WENU AU MTU MWINGINE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUJIBU OMBI HILO.

KAA- MKIJUA KUSHINDWA KUFIKA BARAZA LITASIKILIZA OMBI HILO NA KUTOA UAMUZI BILA NINYI KUWEPO.

IMETOLEWA NAMI KWA AMRI NA CHAPA YA BARAZA LEO TAREHE 13/10/2023.

**MAHELELE MUSA SUKUMBA**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) TARIME**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya GEITA**
**Kituo cha KATORO Mkoa GEITA**
**Shauri la madai/Ndoa Na 81/2023**
**Jina la Mdai: JOYCE JESCAR ROGERS**
**Jina la Mdaiwa: GEORGE OTUOMA GACHO**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuniya 18 ya kanun iza taratibu Madai katika mahakama za Mwanzo)**

**Kwa:GEORGE OTUOMA GACHO WA MWANZA**

Kwa kuwaMdai ameleta madai yake YA TALAKA

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii Tarehe 27 Mwezi 10 Mwaka 2023 saa2.00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO:Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini.Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo Tarehe 10 Mwezi 10 Mwaka 2023

HAKIMU

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Bukoba,**
**Kituo cha Bukoba Mjini Mkoa wa Kagera.**
**Shauri la Madai Na. 28/2023**
**Jina la Mdai ...............NEEMA MWIJAGE**
**Jina la Mdaiwa...........BUTOGWA ELIAS SHUNDA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**Kwa BUTOGWA ELIAS SHUNDA**

Kwa kuwa mdai/wadai ameleta/wameleta madai yake/yao ya talaka, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 19 Mwezi 10 Mwaka 2023 saa 8:30 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/ mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 10 Mwezi 10 Mwaka 2023.

HAKIMU

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KYELA**
**AT KYELA**
**MATRIMONIAL CAUSE NO. 02 OF 2023**
**JUDITH EVARIST...............PETITIONER**
**VERSUS**
**EXAUD MBWILE.............RESPONDENT**

**NOTICE OF PETITION**

Whereas a petition, a copy of which has been presented to this court by the above-named petitioner, will be mentioned before the magistrate on the 6th day of November, 2023 at 8:30 o'clock in the forenoon.

Take notice that all parties to the petition are hereby required to attend before the magistrate on the said day at the said time and that in the event of default by any party to enter appearance , the petition shall be proceeded with in accordance with the provisions of the law of marriage (Matrimonial Proceedings) Rules.

Dated at Kyela this 6th day of October, 2023.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
KYELA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/54)**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MVOMERO**
**WILAYA YA MVOMERO**
**MADAI NAMBARI 31/...2023**
**MDAI: HALIMA IBRAHIMU**
**ANAMDAI**
**MDAIWA: MUSSA IDDI KILINGO**

**KWA: MUSSA IDDI KILINGO**
**WA POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba: MDAI ANADAI TALAKA NA MATUNZO YA MTOTO UNAHITAJIKA KUJA KUJIBU DAI DHIDIYAKO

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa Kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya IJUMAA tarehe 20/10/2023 saa 03:00 ASUBUHI ambapo ni siku ya kusikilizwa madai yako kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuletwa mashahidi wako na hati zote za mashahidi hao kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo

Angalia kama hukudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu Mahakama hii huku ukiwa/mkiwa umepokea/mmepokea kuitwa shaurini, hii inaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa madai yako/yenu.

Hati hii imetolewa kwa Amri na yangu na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 12/10/2023

HAKIMU

---

**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Ya wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI**
**Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la madai/Ndoa Na 1432/2023**
**Jina la mdai MUGEMANA JEAN BOSCO**
**Jina la mdaiwa NDAYAHOZE FLORENTINE**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa NDAYAHOZE FLORENTINE**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za madai) TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 24 Mwezi 10 Mwaka 2023 saa 1:50 asubuhi mbele ya Mhe MWAGENI kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelzo vyote vinavyohusu shauri hili kwaajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila yaw ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 16 Mwezi 10 mwaka 2023

HAKIMU


# Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701


**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.



Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) likijadili suala la Palestina. **PICHA: MTANDAO**

# Israel yakubali kuwasilishwa msaada

- Rais Biden kuitembelea Israel leo
- UNSC yapinga pendekezo la Russia

**TEL AVIV,** Israel

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Marekani Antony Blinken, amesema Israel imekubali kufanya kazi na Marekani na Umoja wa Mataifa (UN) kuhusu kuwasilisha msaada kwa wakazi wa Gaza, huku akibainisha kuwa Rais wa Marekani Joe Biden atatembelea Israel leo kutokana na mashambulizi ya Hamas.

Blinken aliyabainisha hayo jana akiwa Mjini Tel Aviv, baada ya kuwa na mazungumzo ya karibu saa nane na Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, kwenye wizara ya Ulinzi ya Israel, akiwa katika ziara yake ya pili ya nchi hiyo tangu Oktoba saba pale Hamas iliposhambulia taifa hilo.

Alisema Rais Biden atathibitisha tena uungaji mkono wa Marekani kwa Israel na kueleza dhamira zake za dhati kwa ajili ya usalama wa taifa hilo.

"Marekani imepata uhakikisho kutoka kwa Israel juu ya kutayarisha mpango wa kuruhusu msaada wa kigeni kuingia katika kanda iliyozingirwa na yenye hali duni ya Gaza, wakati Israel inajitayarisha kwa uvamizi wa nchi kavu dhidi ya maeneo yanayoshikiliwa na Hamas," alisema.

Mwanadiplomasia mkuu wa Marekani yuko katika siku yake ya tano ya mazungumzo mfululizo na viongozi wa nchi za Mashariki ya Kati, katika juhudi za kutafuta suluhisho kwa mzozo wa Gaza kati ya Israel na Hamas.

Msemaji wa Baraza la Usalama wa Taifa la Marekani, John Kirby alitangaza mjini Washington kwamba Biden atatembelea pia Jordan ambako atakutana na Mfalme Abdullah wa Pili, Rais Mahamoud Abass wa Palestina, na Rais Abdel Fatah al Sisi wa Misri.

> Ilielezwa kuwa katika mkutano wa baraza hilo, baadhi ya wajumbe walikataa kuunga mkono hoja ya kuilaani Hamas pekee yake kwa kufanya shambulio la kushtukiza dhidi ya Israel lililosababisha vifo vya watu 1400.

Kirby aliwaambia waandishi wa habari kwamba Rais Biden atasisitiza tena kwamba Hamas haiwakilishi maslahi ya Wapalestina ya haki yao ya kupata utawala wao, na atazungumzia pia msaada wa dharura kwa rais wa Gaza.

**MAKABILIANO YAONGEZEKA**

Wakati hayo yakiendelea, ilibainishwa kuwa mvutano katika mpaka unaozozaniwa wa Israel na Lebanon unazidi kuongezeka na kuzusha wasiwasi wa kutokea mzozo mpana wa kikanda.

Ilibainishwa kuwa kumekuwa na majibizano ya ufyatulianaji risasi baina ya Israel na wanamgambo wa kundi la Hezbollah nchini Lebanon katika siku za hivi karibuni.

Makabiliano hayo yalianza muda mfupi baada ya kundi la wanamgambo la Hamas ambalo Marekani na UN limeliorodhesha kuwa shirika la kigaidi, kufanya shambulio kubwa dhidi ya Israel.

Siku iliyofuatia vyanzo nchini Lebanon viliripoti mashambulizi ya Israel yaliyoelekezwa kusini mwa nchi hiyo huku maganda ya risasi yakianguka kwenye kijiji cha Khiam.

Kundi la Hezbollah la nchini Lebanon ambalo linaungwa mkono na Iran tangu wakati huo limedai kuhusika na mashambulizi kadhaa ya roketi kaskazini mwa Israel, huku jeshi la Israel IDF nalo, likijibu mapigo kwa kuyalenga maeneo zaidi upande wa kusini wa Lebanon na kuwaua wanamgambo kadhaa wa Hezbollah.

Ilielezwa kuwa makabiliano hayo ndio makubwa tangu vita vya Lebanon vya mwaka 2006 ambavyo vilisababisha wanamgambo 250 wa Hezbollah na Walebanon zaidi ya 1,000 kuawa sambamba na askari 160 wa Israel.

Aidha, ilibainishwa kuwa kundi la Hezbollah ambalo linajiendesha kama chama cha kisiasa likiwa na viti zaidi ya 60 katika bunge la Lebanon, pia limekuwa na tawi la wapiganaji ambalo linamiliki idadi kubwa ya roketi pamoja na maelfu ya wapiganaji walio na uzoefu.

Kikosi cha muda cha Umoja wa Mataifa nchini Lebanon UNIFIL kilisema kwamba wameshuhudia majibizano makali ya risasi baina ya Lebanon na Israel haswa baada ya makao yake makuu kwenye mji wa Naquora kushambuliwa vikali.

Mapema siku hiyo hiyo, kundi la Hezbollah lilidai kuhusika na shambulio la kombora dhidi ya Israel na kumuua mtu mmoja katika mji wa mpakani wa Shtula.

Kundi hilo lilisema kwamba shambulio hilo lilikuwa ni ulipaji kisasi wa shambulizi la Israel ambalo lilipiga kundi la waandishi wa habari karibu na kijiji cha Alma-al-Shaab, na kusababisha kifo cha mwandishi wa shirika la habari la Reuters, huku watano wakijeruhiwa.

**WANANCHI WAHAMISHWA**

Jeshi la Israel lilitangaza kwamba takribani jamii 30 zilizoko ndani ya kilometa mbili kwenye mpaka wake wa kaskazini na Lebanon zitahamishwa na kulitaja kuwa eneo la kijeshi.

Eneo la mpaka baina ya Lebanon na Israel bado limesalia kuwa tete na lenye kuzozaniwa huku makabiliano ya mara kwa mara yakizuka, ikielezwa kuwa hakuna mpaka rasmi baina ya nchi hizo mbili na badala yake kumekuwepo na mstari unaotambua mipaka unaoitwa mstari wa buluu, ambao una alama ya mapipa.

Ilibainishwa kuwa mpaka huo ulianzishwa na Umoja wa Mataifa katika miaka ya 2000 ili kuthibitisha kuondoka kwa vikosi vya Israel katika maeneo yanayokaliwa kusini mwa Lebanon.

**MSIMAMO WA UNSC**

Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa (UNSC) limepinga mswada wa azimio uliowasilishwa na Russia unaolaani ghasia zinazoendelea Mashariki ya Kati.

Ilielezwa kuwa katika mkutano wa baraza hilo, baadhi ya wajumbe walikataa kuunga mkono hoja ya kuilaani Hamas pekee yake kwa kufanya shambulio la kushtukiza dhidi ya Israel lililosababisha vifo vya watu 1400.

Pia inaelezwa kuwa baraza lilishindwa kupitisha mswada wa azimio, wakati Israel ikijitayarisha kufanya shambulio la nchi kavu baada ya mashambulio makubwa ya anga ya mabomu ambayo maofisa wanasema yamesababisha vifo vya karibu watu 2,750.

Hata hivyo, ilibainishwa kuwa ni mataifa manne pekee yaliyounga mkono pendekezo la Russia, mataifa mengine manne yaliungana na Marekani kupinga na mataifa sita hayajaunga mkono upande wowote.

Wanadiplomasia kwenye Umoja wa Mataifa wanasema pendekezo jingine ambalo limetayarishwa na Brazil ambalo linatumia lugha ya kulaani kundi hilo la wanamgambo wa kiislamu linaonekana litapata uungaji mkono zaidi na linatazamiwa kuwasilishwa kupigiwa kura siku chache zijazo.

**VOA, DW**

# AZAM YAONGOZA MABAO YA VICHWA LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

AZAM FC ndiyo timu pekee iliyofunga mabao mengi ya vichwa (mawili) kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ipo katika raundi ya tano mpaka sasa.

**Kwa mujibu wa takwimu za Dawati la Michezo la Nipashe ni mabao manane ya vichwa yamefungwa mpaka sasa, ambapo kati ya hayo Azam imefunga mawili kupitia wachezaji wake Idd Selemani 'Nado' na Feisal Salum.**

Feisal alifunga bao la kichwa Agosti 16, Azam ilipoisulubu Tabora United mabao 4-0, wakati Nado alifanya hivyo Septemba 21, mwaka huu, akipachika bao la pili la ushindi, Azam ikiifunga Singida Fountain Gate 2-1, Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Timu nyingine zenye mabao yaliyofungwa kwa kichwa ni Simba, bao lake likiwekwa wavuni na Fabrice Ngoma kwenye mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro, Simba ikipata ushindi wa mabao 4-2 Agosti 15, mwaka huu.

Zingine ni JKT Tanzania kupitia Edward Songo, KMC wakifungiwa na Juma Shemvuni, Namungo kwa bao la Pius Buswita, Geita Gold kwa bao la Elius Maguri, na Ihefu ambayo bao lake la kichwa lilifungwa na Lenny Kisu kwenye mechi ambayo ilishinda mabao 2-1 dhidi ya Yanga.



Timu ambazo mpaka sasa hazijaonja ladha ya mabao ya vichwa ni Yanga, Mashujaa, Singida Fountain Gate, Coastal Union, Mtibwa Sugar, Kagera Sugar, Tabora United, Prisons na Dodoma Jiji.

Wakati huo huo takwimu zikionyesha mpaka sasa penalti sita zimetoka, tano zikiwekwa wavuni, ambapo Bodi ya Ligi imetoa majina ya wachezaji sita waliosababisha penalti hizo.

Wachezaji hao ni Moses Phiri na Luis Miquissone wa Simba, Shiza Ramadhani 'Kichuya' wa Namungo, Antony Mlingo wa Geita Gold, Edson Katanga wa JKT Tanzania na Impiri Mbombo wa Tabora United.

Kwa mujibu wa takwimu zetu, penalti hizo ziliwekwa wavuni na Fabrice Ngoye wa Namungo, Jean Baleke na Saidi Ntibazonkiza wa Simba, Daniel Lyanga wa JKT Tanzania na Erick Okutu wa Tabora United, huku Elius Maguri wa Geita Gold akikosa penalti yake.

## *Zawadi Sanya Sanya na M-Bet zaanikwa*

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Michezo ya Kubahatisha ya M-Bet Tanzania, imezindua kampeni mpya ijulikanayo kwa jina la Sanya Sanya na M-Bet, ambayo itamwezesha mshindi kushinda fedha taslimu, simu ya mkononi na televisheni ya kisasa (Smart TV).

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa kampeni hiyo jana jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi, alisema lengo la kuanzisha kampeni hiyo ni kuwazawadia wateja wao kuelekea kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Mushi alisema wameanza kampeni mapema zaidi kwa lengo la kuwazawadia wateja wao wengi na kubadili maisha yao.

Alisema kwa wateja wa M-Bet Tanzania wenye simu za kawaida maarufu kama 'kitochi', wanatakiwa kutumia USSD menyu yao kwa kupiga *149*19# na kuanza kubashiri matokeo ya mechi kuanzia mbili za ligi mbalimbali duniani.

Mushi alisema mbali ya kutumia USSD menyu hiyo, pia wanaweza kubashiri kwa kutumia app ambayo lazima uipakue kwa watumiaji wa simu janja (smartphone).

Alisema wateja wao watakaoweka dau kuanzia Sh. 5,000 na kubashiri kuanzia mechi mbili katika masoko yote ya kampuni ya M-Bet Tanzania kama Perfect 12, Normal, Dakika 45 na Multibet, watashinda zawadi ya televisheni ya kisasa (Smart TV) ambapo droo yake itafanyika kila wiki.



Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro (kushoto), akimkabidhi Mwigizaji wa Filamu, Jacob Steven 'JB', Tuzo ya Hollywood and African Prestigious (Hapawards) 2023, kutoka nchini Marekani katika Kipengele cha Mwigizaji Bora wa Filamu (Best Bongo Movie Actor), zilizofanyika hivi karibuni nchini Marekani. **NA MPIGAPICHA WETU**

## GBT kuadhimisha miaka 20 kwa bonanza Dar

**Faustine Feliciane**

BODI ya Michezo ya Kubahatisha nchini (GBT), imeandaa bonanza maalum kwa wadau wake kwa ajili ya kuadhimisha miaka 20 tangu kuanzishwa kwake, imeelezwa.

Bonanza hilo litafanyika Jumamosi wiki hii Masaki jijini Dar es Salaam, litahusisha michezo ya mpira wa miguu, netiboli, kuvuta kamba pamoja na kukimbiza kuku.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mkurugenzi Mkuu wa GBT, James Mbalwe, alisema pamoja na kuadhimisha miaka 20 tangu kuanzishwa kwa bodi hiyo, pia bonanza hilo litawapa nafasi ya kukutana pamoja wafanyakazi wa bodi, wadau wa bodi hiyo na wadhamini wao.

"Lakini pia ni sehemu ya kuwashukuru wadau wetu kwa kuwa nasi kwa kipindi chote hiki," alisema Mbalwe.

Aidha, Mwenyekiti wa Chama cha Waendesha Michezo ya Kubashiri Tanzania, Sabrina Msuya (pichani chini), alisema wanatarajia bonanza hilo litashirikisha makampuni 15 yanayofanya kazi na bodi hiyo.

Alisema mbali na kufanyika kwa bonanza hilo, pia wanatarajia kutoa misaada kwenye Hospitali ya Ocean Road kuelekea Oktoba 27 siku ya kilele cha maadhimisho hayo ya miaka 20 tangu kuanzishwa kwa bodi hiyo.

"Oktoba 26 ndio siku tutakayokwenda kutoa misaada katika Hospitali ya Ocean Road, lakini siku inayofuata tunatarajia kuwa na mkutano wa wadau wote wa michezo ya kubahatisha na bahati nasibu, lengo ni kuangalia namna gani tunaendelea kushirikiana na GBT na kuwawezesha kufikia malengo kama Serikali," alisema Sabrina.

Bodi ya michezo ya kubahatisha Tanzania ilianzishwa mwaka 2003 chini ya sheria ya michezo ya kubahatisha kifungu namba 41.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MOURINHO KUONDOKA ROMA

KOCHA wa AS Roma, Jose Mourinho, anatarajiwa kuondoka katika klabu hiyo ya Italia mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu, hakuna mazungumzo yaliyofanywa kuhusu kuongezwa kwa mkataba wake. ***(Sky Sports Italia, Football Italia)***

### CONTE AITAMANI NAPOLI

KOCHA wa zamani wa Juventus, Chelsea na Tottenham Hotspurs, Antonio Conte, amesema siku moja angevutiwa kuinoa Roma au Napoli, na kwamba aliikataa Timu ya Taifa ya Saudi Arabia. ***(Il Corriere della Sera, Football Italia)***

### HOJBJERG AWINDWA JUVE

JUVENTUS inaendelea kumfuatilia kiungo wa kati wa Denmark, Pierre-Emile Hojbjerg, 28. ***(La Gazzetta dello Sport)***

### GUEHI ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inapania kumnunua beki wa Crystal Palace na England, Marc Guehi, 23, ambaye amekuwa akihusishwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu England. ***(Football Insider)***

### BAILEY MKATABA MPYA

KLABU ya Aston Villa inafikiria kumpa Leon Bailey, 26, mkataba mpya, huku mkataba wa sasa wa winga huyo wa Jamaica ukikamilika Juni 2025. ***(Football Insider)***

### KUONGEZEWA MKATABA

KLABU ya Arsenal ina uhakika wa kukubaliana mkataba mpya na beki wa England, Ben White, 26, ambaye ana furaha katika klabu hiyo. ***(Fabrizio Romano)***

### MAATSEN AWINDWA CITY

MANCHESTER City na West Ham zinatarajiwa kumsajili beki wa Uholanzi, Ian Maatsen, 21, ikiwa mchezaji huyo ambaye amekuwa akihusishwa na Barcelona, hatasaini mkataba mpya Chelsea baada ya mwisho wa msimu huu. ***(Teamtalk)***

### GASSOVA AIVUTIA EVERTON

KLABU ya Everton inavutiwa na winga wa Corinthians na Brazil, Wesley Gassova, 18, lakini watakabiliwa na ushindani. ***(Teamtalk)***

### THIAW KUBAKI MILAN

MLINZI wa kati wa Ujerumani, Malick Thiaw, 22, anataka kubaki AC Milan licha ya kutakiwa na Real Madrid na West Ham. ***(Calcio Mercato)***

### KONE MWAKA MMOJA

BORUSSIA Monchengladbach itaanzisha kipengele cha kuongeza mkataba na kiungo Mfaransa, Manu Kone, 21, kwa mwaka mmoja ili uendelee hadi 2026. ***(Rheinische Post, via Get German Football News)***

### LAVIA HADI NOVEMBA

KIUNGO wa kati wa Ubelgiji, Romeo Lavia, 19, ambaye bado hajacheza mechi yake ya kwanza Chelsea tangu ajiunge nayo kutoka Southampton msimu wa majira ya joto, anatarajiwa kuwa nje ya uwanja hadi mwisho wa Novemba kutokana na jeraha la kifundo cha mguu alilolipata akiwa mazoezini. ***(Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR ATETEWA

**SAO PAULO,** Brazil

### Ni baada ya kurushiwa 'popcorn' na mashabiki kutokana na kutofurahishwa na...

MSHAMBULIAJI wa Real Madrid, Rodrygo, amemtetea mchezaji mwenzake wa kimataifa Neymar kuwa nyota huyo wa Al Hilal bado ndiye "mchezaji mkuu wa Brazil".

**Neymar alirushiwa mfuko wa bisi (popcorn) kutoka kwa mashabiki baada ya sare ya bao 1-1 Alhamisi iliyopita nyumbani dhidi ya Venezuela, tukio ambalo kocha wa Brazil, Fernando Diniz, alilaani. Na jana Jumanne Brazil ilitarajiwa kucheza na Uruguay huko Montevideo kwenye mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia.**

Mashabiki wa Brazil walichanganyikiwa na matokeo hayo na Neymar - ambaye anaonekana kama 'hirizi' ya nchi hiyo kwa muda mrefu - alibeba mzigo wa ukosoaji huo.

"Haibadilishi chochote ikiwa (Neymar) ana umri wa miaka 31 au la, anaendelea na ubora kama kawaida," alisema Rodrygo kabla ya mchezo wa jana.

"Anabaki kuwa mchezaji wetu mkuu. Bila shaka, tunapopoteza au sare kwenye mchezo, jukumu litakuwa kubwa kwake, lakini tunaposhinda, inakuwa wazi kuwa ni mchezaji wetu bora na tunamtegemea sana."

Dhidi ya Venezuela, Neymar alimtengenezea pasi Gabriel Magalhaes aliyefunga bao la Brazil, huku yeye akikosa nafasi kadhaa za wazi.

Rodrygo mwenye umri wa miaka 22, alimsifu Neymar ambaye mwezi uliopita alimpita Pele na kuwa mfungaji bora wa muda wote wa wanaume wa Brazil akiwa na mabao 79 katika mechi 125 za kimataifa.

"Ni muhimu sana uwanjani na nje ya uwanja pia," alisema Rodrygo kuhusu fowadi huyo wa zamani wa PSG na Barcelona.

"Kama wanavyomsema vibaya kila mara, watu wanaoishi naye kwa ukaribu wanajua kwamba yeye ni tofauti kabisa na sura ambayo baadhi ya watu wanamuona.

"Yeye huwa anazungumza nami kila mara. Wakati mwingine nipo kwenye klabu yangu, yeye yuko huko (Saudi Arabia) na ananitumia ujumbe, ananiambia mambo chanya. Kwa hiyo ushauri huo wa nje ya uwanja unatuathiri sana na hutusaidia sana uwanjani."

Neymar, wakati huo huo, anaelewa kufadhaika kwa mashabiki wa Brazil, lakini alikasirishwa na tukio la kutupiwa mfuko wa bisi.

"Inasikitisha, ni wazi inasikitisha sana," alisema Neymar.

"Nalaani tabia hiyo, si lazima uifanye, ni mbaya sana kwa mpira wa miguu na kwa wanadamu, siji likizo hapa, zaidi ya kutembea, nimekuja kufanya upendo zaidi kwa kucheza mpira wa miguu na kutetea nchi yangu.

"Ni wazi, tuko pale tukifanya tuwezavyo, tukitoa tuwezavyo, na mara nyingi matokeo hayaji, na sivyo mashabiki wanavyotarajia."

Matokeo hayo yaliiacha Brazil nafasi ya pili katika kundi lao la timu 10 za kufuzu kwa michuano ya Amerika Kusini kwa pointi saba kutokana na michezo mitatu, pointi mbili nyuma ya mabingwa wa Kombe la Dunia, Argentina.

Neymar na Brazil watarejea uwanjani Jumanne katika mechi nyingine ya kuwania kufuzu michuano hiyo.



# TEN HAG YUPO KWENYE MIPANGO YA RATCLIFFE

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag atapata uhakikisho wa kuwa sehemu ya mipango ya Sir Jim Ratcliffe kwa Manchester United ikiwa bilionea huyo wa England atafikia makubaliano ya kuongoza idara ya michezo ya klabu hiyo, kwa mujibu wa ESPN.

Ratcliffe, mwanzilishi wa Kampuni ya Kemikali ya INEOS, ana matumaini ya kupata asilimia 25 ya hisa za klabu hiyo badala ya uwekezaji wenye thamani ya karibu pauni bilioni 1.3.

Ana nia ya kuwa na ushawishi juu ya uendeshaji wa soka, lakini mabadiliko yoyote yaliyopendekezwa hayatajumuisha kuchukua nafasi ya Ten Hag.

Mholanzi huyo aliiongoza United kumaliza katika nafasi ya tatu kwenye Ligi Kuu ya England na kushinda Kombe la Carabao katika msimu wake wa kwanza kufuindisha.

Licha ya kuanza vibaya kwa kampeni ya sasa ambapo United wamepoteza mechi sita kati ya 11 katika mashindano yote, Ratcliffe ana mpango wa kumbakisha Ten Hag kama kocha.

United wanatazamiwa kufanya mkutano wa bodi kesho, Alhamisi wakati makubaliano na Ratcliffe na INEOS yanaweza kukamilishwa.

Ratcliffe anafahamu kuwa ofa yake ya kununua hisa chache inaweza kuwa isiyopendwa na mashabiki kwa sababu bado familia ya Glazer ndio inayoimiliki kwa asilimia kubwa.

Ana matumaini kwamba kwa kupata hisa asilimia 25 ya klabu, itafungua milango ya kuinyakua zaidi angalau kwa muda mfupi.

Mashabiki walikuwa na nia kuona umiliki wa miaka 18 wa Glazers ukiisha ilipotangazwa mnamo Novemba kuwa familia hiyo kutoka nchini Marekani inaweza kuiuza, lakini Jumamosi ilifichuliwa kuwa ofa moja ya udhibiti wa klabu hiyo kwa asilimia 100 kutoka kwa Sheikh Jassim ilikuwa imeondolewa.

Mfanyabiashara huyo wa Qatar alijiondoa katika mchakato huo wiki iliyopita akitaja hesabu ya "ushabiki" ya Glazers kama sababu kuu.

Ofa ya mwisho ya Sheikh Jassim ilikuwa na thamani ya karibu pauni bilioni tano, ikiwa ni pungufu ya pauni bilioni moja bei iliyokuwa ikitakiwa na Glazers.

# Kocha Argentina hafikirii Messi kustaafu

**BUENOS AIRES,** Argentina

KOCHA wa Argentina, Lionel Scaloni, hafikirii kama Lionel Messi atastaafu kuichezea timu hiyo ya taifa hivi karibuni.

Messi mwenye umri wa miaka 36, alikuwa nahodha wa Argentina na kutwaa ubingwa wa Dunia 2022 huku akishinda Mpira wa Dhahabu, lakini hajatoa maelezo yoyote kuhusu lini atastaafu soka ya kimataifa.

Alipoulizwa katika mkutano na waandishi wa habari Jumatatu kabla ya mechi ya Argentina ya kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya Peru ikiwa anapaswa kuzoea kucheza bila Messi, Scaloni alisema: "Tukumbuke kwamba yeye (Messi) bado yuko hapa. Njia gani ya kufikiria 'anapokuwa amekwenda.' Ukweli ni kwamba bado yupo, tumuache."

Messi aliingia akitokea benchi na kucheza kwa zaidi ya dakika 40 katika ushindi wa bao 1-0 wa Argentina dhidi ya Paraguay katika mechi ya kufuzu Kombe la Dunia Alhamisi. Mshambuliaji huyo wa Inter Miami CF alifunga katika ushindi wa bao 1-0 mwezi uliopita dhidi ya Ecuador, lakini akakosa mechi ya pili ya kufuzu la Kombe la Dunia ya ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Bolivia kutokana na matatizo ya misuli.

"Leo Messi yuko sawa," alisema. "Amekuwa akiongeza dakika za mazoezi, tutafanya uamuzi kesho, ni suala la dakika, ni kiasi gani anaweza kucheza. Ikiwa yuko vizuri, unajua ninachofikiria, atacheza.

"Siku zote tunajaribu kucheza zile ambazo ziko kwa asilimia 100 au karibu na asilimia 100. Leo ni vigumu sana kwa kila mtu kuwa katika ubora wake katika michezo hii, hivyo kunaweza kuwa na tofauti kuhusiana na mchezo dhidi ya Paraguay."

Messi atamaliza msimu wa MLS Oktoba 22 ugenini kwa Charlotte baada ya Miami kushindwa kufuzu mchujo. Klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Marekani, MLS, itacheza mechi mbili nchini China Novemba, mwaka huu.

# TP Mazembe, Esperance rasmi kwa Mkapa

**Na Saada Akida**

WAZIRI wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, amesema baada ya kupata heshima ya ufunguzi wa mashindano ya African Football League, Tanzania imepata tena nafasi ya kuwa mwenyeji wa mchezo wa pili kati ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Esperance ya Tunisia.

Akizungumza na Nipashe jana, Ndumbaro alisema maandalizi yanaendelea vizuri kwa viwango vya Shirikisho la Soka duniani (FIFA), sehemu ya kuchezea na waandaaji wamefurahishwa na ukarimu wa Watanzania katika kupokea mizigo na masuala mengine ya kiusalama.

Alisema kutokana na maagizo kutoka Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), wamewapa nyongeza ya mechi kati ya TP Mazembe na Esperance ya Tunisia iliyopaswa kuchezwa Lubumbashi nchini DR Congo, ambapo sasa mechi hiyo imehamishiwa Dar es Salaam.

"Mechi hii itapigwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Oktoba 22 (Jumapili), heshima ya Rais Samia Suluhu Hassan, inazidi kuongezeka mechi ya ufunguzi hapa na mechi ya pili pia itapigwa hapa.

"Ni heshima kwa Tanzania kwa maandalizi mazuri ambayo Watanzania tumeyafanya na Afrika Football League, lakini kwa heshima ambayo Rais Samia Suluhu Hassan ametupa Watanzania pamoja na FIFA na CAF," alisema Ndumbalo.

Aliongeza kuwa Serikali kwa kushirikiana na Shirikisho la Mpira wa Miguu nchini (TFF) pamoja na Afrika Football League, FIFA na CAF, wameanza maandalizi hayo kwa ajili mechi ya Oktoba 22, na wanaomba Watanzania waujaze tena Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Nilisema awali naomba nirudie hicho ndio kigezo cha sisi kupewa mechi ya ufunguzi na fainali za Mataifa ya Afrika 2027, hivyo nawaomba Watanzania tujipange na tujiandae na mchezo kati ya TP Mazembe na Esperance, ni fursa kwetu kutangaza nchi kiuchumi, kijamii na utalii," alisema Dk. Ndumbaro.



# BENJAMIN MKAPA WAKAMILIKA 99%

**Na Saada Akida**

UWANJA wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, sasa umekamilika kwa asilimia 99 na tayari kwa ajili ya mechi ya ufunguzi rasmi wa mashindano ya African Football League (AFL) Ijumaa wiki hii.

**Mashindano hayo yanatarajiwa kuanza kutimua vumbi Ijumaa kwa Simba kucheza mechi ya ufunguzi dhidi ya Al Ahly ya Misri katika Uwanja wa Mkapa majira ya saa 12:00 jioni.**

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja wa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Milinde Mahona, alisema awamu ya kwanza ya ukarabati wa uwanja umekamilika kwa asilimia kubwa na wanatarajia ndani ya siku chache kukamilika asilimia hiyo moja.

Alisema uwanja huo utafunguliwa rasmi kwa ajili ya michuano ya AFL na utaendelea kutumika katika michezo hiyo baada ya hapo utaendelea kufanyiwa marekebisho kwa awamu ya pili.

"Katika awamu ya pili utakuwa ni kufumua uwanja eneo la kuchezea na sehemu ya kukimbilia riadha, hiyo ni awamu ya pili kwa ajili ya kujiandaa na uwenyeji wa mashindano mbalimbali ikiwamo AFCON 2027.

"Lakini kabla ya kufanya ukarabati wa awamu ya pili itafanywa tathmini baadaye maamuzi yatatolewa kama Simba au Yanga kuweza kutumia uwanja huu katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika," alisema meneja huyo.

Aliongeza kuwa serikali inafanya jitihada za kuhakikisha ukarabati wa awamu ya pili unafanyika kwa haraka ili klabu hizo na timu za taifa kuweza kutumia uwanja katika mashindano makubwa.

Kuhusu changamoto za maji hasa vyooni, alisema limefanyiwa kazi na halitajirudia tena kwa sababu wamekuwa makini kufanyia maboresho kila sehemu ambayo ilikuwa na shida.

"Sehemu ya waandishi imetengwa na kufanyiwa maboresha hawataingiliwa na mashabiki kama ilivyokuwa awali kwa sababu ni maalum kwa ajili ya kufanya kazi zao.

"Hizo nazo zimefanyiwa kazi pia kikubwa ni mashabiki nao kuweza kufuata taratibu na kuingia uwanjani mapema kuepuka msongamano wa milangoni na mageti," alisema Meneja.

Suala la viti kuwekwa namba na mashabiki kukaa sehemu husika, Mahona alisema kwa sasa utaratibu utakuwa kama awali hadi hapo ukarabati wa awamu ya pili utakapofanyika.

"Nakiri awali kulikuwa na changamoto ya taa, umeme ukikatika, unaporejea inachukua dakika 25 hadi 15 kuwaka, sasa tumeboresha kwa kufungwa taa mpya kama itatokea changamoto zozote za umeme basi zitawaka kwa haraka sana.

Pia, tumenunua jenereta kwa ajili ya sehemu ya kucheza ya uwanja, lakini tumezungumza na Shirika la Umeme nchini (TANESCO), kusiwapo kwa mgao wa umeme katika eneo hilo," alisema Mahona.

Alisema utaratibu ni kwamba timu inayohitaji kutumia uwanja itawasiliana na TFF kupewa mwongozo ambao wataandika barua kwa Katibu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo kuangalia uwezekano wa siku hiyo kupatikana kwa uwanja.

Meneja huyo alisema gharama za kukodi uwanja huo ni Sh. milioni 20, iwe timu zote za ndani au nje, mfano Simba au Yanga katika sherehe zao basi watatoa kiasi hicho ikiwamo mechi za ligi au kimataifa wanalazimika kutoa asilimia 15 ya mapato ya mechi.

Alisema baada ya mechi ya Simba na Al Ahly, Jumapili kutakuwa na mchezo wa TP Mazembe DR Congo ambao watakuwa wenyeji wa Esperance ya Tunisia, hivyo serikali itaingiza kiasi cha Sh. milioni 20 kutoka kwa mwenyeji wa mchezo huo kama gharama ya kuukodi.

**KWA WAANDISHI...**



Mafundi wakiendelea na marekebisho ya eneo watakalokuwa wanakaa waandishi wa habari katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya maandalizi ya mashindano ya African Football League yanayoanza Ijumaa wiki hii kwa mechi kati ya Simba na Al Ahly ya Misri. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Phiri mkataba mnono Simba

INATOKA UKURASA 24

Simba ilimsajili straika huyo msimu uliopita kutoka Zanaco ya Zambia na alikuwa tegemeo upande wa upachikaji mabao akiiwezesha kutinga makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu uliopita, akifunga mabao mechi zote za hatua za mwanzo dhidi ya Nyasa Big Bullets ya Malawi na Primeiro de Agosto ya Angola, kabla ya kutolewa kwenye hatua ya robo fainali dhidi ya Wydad Casablaca akiwa tayari ni majeruhi.

Aliumia Desemba 21, mwaka jana kwenye mechi ya Ligi Kuu msimu uliopita Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, timu yake ikicheza dhidi ya Kagera Sugar, mchezo ukimalizika kwa sare ya bao 1-1 na kukaa muda mrefu ambapo kwa siku za karibuni ameanza kuwa fiti baada ya kutoka majeruhi akipata nafasi ya kuingia kama mchezaji wa akiba.

Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo alisema hakuna mchezaji yeyote ambaye Simba itataka abaki akaondoka.

Alisema mchezaji yeyote kama anatakiwa na klabu hiyo basi atabaki, hivyo wanachama na mashabiki wa timu hiyo wasiwe na wasiwasi kuhusu mchezaji muhimu kuondoka klabuni hapo.

"Ukiona mchezaji ameondoka Simba ujue ameuzwa kwenda kwenye klabu kubwa zaidi Afrika na kutuingizia pesa nyingi, au haimhitaji hivyo imempa ruhusa akatafute maisha mengine na si vinginevyo," alisema Ahmed.

Habari zinasema kwa sasa klabu hiyo imeanza mchakato wa kuwaongezea mikataba wachezaji wote inaowahitaji ambao watamaliza mikataba yao mwishoni mwa msimu huu.

## Jamhuri yaipania JKU Ligi Z'bar leo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya soka ya Jamhuri, imesema kuelekea mchezo wake wa leo dhidi ya maafande wa JKU, imejipanga na kudhamiria kupata alama tatu wakiwa katika Uwanja wao wa nyumbani Kisiwani Pemba.

Mchezo huo utakaochezwa katika dimba la Finya majira ya saa kumi alasiri ni mwendelezo wa Ligi Kuu Zanzibar katika mzunguko wake wa saba.

Jamhuri SC inashuka uwanjani ikiwa imeanza vibaya Ligi Kuu Zanzibar kwa kushinda mchezo mmoja tu, sare tatu na ikipoteza mechi mbili katika michezo sita iliyocheza wakati huu ikiwa nafasi ya 11 katika msimamo wa ligi hiyo baada ya kujikusanyia pointi sita.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Juma Abdallah, alisema mchezo huo utakuwa mgumu kwa kuwa wapinzani wao walipoteza mchezo uliopita, hivyo watakuja na mbinu mbadala za kuweza kuwapata matokeo.

Alisema kama mwalimu amekiandaa kikosi chake kukabiliana na hali yoyote uwanjani ikiwamo wachezaji kuusoma mchezo mapema ili wapate matokeo mazuri.

Alisema anawajua JKU vizuri na msimu huu malengo yao wameelekeza katika ubingwa, hivyo lazima wacheze kwa kujihami na tahadhari.

"Hatukuanza vizuri Ligi Kuu, michezo mitatu ya mwanzo tulicheza ugenini katika Uwanja wa Mau Kisiwani Unguja, ambapo hatukufanya vizuri, hivyo mkakati wetu ni kuhakikisha uwanja huu wa nyumbani tunapata alama tatu ili kujiweka katika nafasi za juu kwenye msimamo wa ligi,"alisema.

## Yanga kuitumia mechi Simba kuimaliza Al Ahly

INATOKA UKURASA 24


wa ni ya ufunguzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Timu zingine zinazoshiriki michuano hiyo AFL ni pamoja na Wydad Casablanca (Morocco), Mamelodi Sundowns (Afrika Kusini), Esperance Tunis (Tunisia), Petro Atletico de Luanda (Angola), Enyimba FC (Nigeria) na TP Mazembe (DR Congo).

# Michezo

Jumatano Oktoba 18, 2023

Nipashe



## Kocha hafikirii Messi kustaafu

UKURASA 22

KWA MKAPA KAMILI 99%...



Mwonekano wa Uwanja wa Benjamin Mkapa, ukiwa katika marekebisho makubwa kuelekea mashindano ya African Football League, ambapo mechi ya ufunguzi itapigwa Ijumaa wiki hii kati ya wenyeji Simba watakaoikaribisha Al Ahly ya Misri. **HABARI UK. 23. PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga kuitumia mechi Simba kuimaliza Al Ahly

## ●●● Gamondi na benchi zima kuhamia kwa Mkapa Ijumaa na 'diary' zao...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Simba ikitarajia kucheza mechi ya ufunguzi ya michuano ya African Football League (AFL) keshokutwa, Ijumaa dhidi ya Al Ahly ya Misri, benchi la ufundi la Yanga nalo linajipanga kwa ajili ya kuhakikisha linautazama kwa makini mchezo huo kwa ajili ya kupata mbinu za kucheza na timu hiyo katika mchezo wao wa hatua ya makundi wa Ligi ya Mabingwa Afrika.

Taarifa zilizopatikana ndani ya kambi ya timu hiyo jana, zimeeleza kuwa Kocha Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi na timu yake ya wataalam wa kuchambua na kusoma mbinu za michezo ya wapinzani, watakuwa uwanjani siku hiyo kwa kazi moja tu ya kuratibu kila kitu kinachoendelea, ikiwamo mfumo watakaoutumia na hata kujua wachezaji hatari wa kuchungwa.

Habari zimeeleza kuwa benchi la ufundi la Yanga limeamua kuutumia mchezo huo kwa sababu mechi wakatayocheza Desemba Mosi, mwaka huu itakuwa hapa nchini, hivyo wana uhakika kuwa watapata uwezo sahihi wa Al Ahly wanapocheza ugenini ikiwamo kuhimili hali ya hewa ya Dar es Salaam.

**"Kila kitu watakachofanya hapa kwenye mechi dhidi ya Simba kitakuwa sahihi kwetu kujifunza kwa sababu hawatobadilika wakija tena kucheza hapa, mfumo watakaotumia, spidi yao, na hata uhimili wa hali ya hewa ya hapa," kilisema chanzo hicho.**

Yanga ipo Kundi D pamoja na Al Ahly, CR Belouzdad ya Algeria na Medeama ya Ghana.

"Ni kweli Simba inacheza dhidi ya Al Ahly kwenye michuano ya AFL, lakini pambano hili linaweza kuwa na manufaa makubwa kwa Yanga, kwa sababu baada ya hapo tayari tutakuwa tumeshajua uimara na udhaifu wa Al Ahly hii mpya, hasa ikicheza ugenini kwenye maeneo ya joto kama haya," alisema mtoa habari huyo.

Naye Makamu wa Rais wa klabu hiyo, Arafat Haji, ametamba kuwa kwa sasa wana kikosi kizuri ambacho kinaweza kushindana na timu kubwa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikiwamo Al Ahly.

"Al Ahly ni timu nzuri na itakuwa inatetea ubingwa, lakini sisi tunatakiwa kuonesha kwamba tunastahili kushindana nao na kushinda mechi ya nyumbani na ugenini, tuna kikosi kizuri cha kupambana nao," alisema Arafat.

Alisema kama uongozi siku zote wameendelea kulipa benchi la ufundi uhuru na mahitaji muhimu na wameendelea kuliamini.

Timu yetu ipo tayari kwa Ligi ya Mabingwa, tuna wachezaji katika Timu ya Taifa ya Tanzania na wapo wachezaji wengine wenye uzoefu wa kutosha, hivyo tunaamini pia tunaweza kufanya vizuri kwenye michezo yetu ya Kundi D tulilopangwa," alisema.

Simba ni timu pekee katoka Ukanada wa Afrika Mashariki (CECAFA), ambayo inashiriki michuano hiyo AFL inayoshirikisha timu nane bora zaidi barani Afrika huku mechi yao dhidi ya Al Ahly iki-

INAENDELEA UKURASA 23

# Phiri mkataba mnono Simba

**Na Adam Fungamwango**

STRAIKA wa Simba Moses Phiri yupo kwenye hatua za mwisho kuongeza mkataba mnono wa miaka miwili na timu hiyo.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zimeeleza kuwa Phiri baada ya mazungumzo marefu, amekubali kuongeza mkataba na klabu hiyo licha ya kupata ofa nono kutoka klabu zingine moja ya ndani hapa nchini na zingine nje zilizoonesha nia ya kumsajili.

"Phiri katupa kipaumbele sisi ili aongeze mkataba, tumempa ofa ya mkataba wenye vipengele vinne, amevisoma, amekubaliana na sisi, lakini bado hajasaini, ila tunajua wakati muafaka ukifika atafanya hivyo," kilisema chanzo ndani ya klabu hiyo.

Inasemekana kuwa Phiri ambaye anamaliza mkataba wake msimu huu ameonesha kuridhishwa na mazingira yaliyopo kwenye klabu hiyo, pamoja na kupata mapenzi makubwa kutoka kwa wanachama na mashabiki wa timu hiyo.

"Ana amani na ameonekana kupenda mazingira ya klabu pamoja na nchi kwa ujumla, yenye mashabiki wanaopenda sana soka, mwenyewe akiwapenda sana mashabiki wa Simba kwa jinsi wanavyompa sapoti siku zote, hata kwenye nyakati ngumu alizopitia, ikiwamo kuwa majeruhi kwa muda mrefu," alisema mtoa taarifa.

INAENDELEA UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >